**Mambo** manane yatakayofanya mama mkwe akuchukie

UKURASA 11



**Uasi** waitikisa Russia, Wagner wateka kambi za jeshi,-miji

UKURASA 17


MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
MAISHA NI NYUMBA
VITUMBUA VYA NAZI
HARUSI
FULANA INAPENDEZA

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 25, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581352

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Samia: Mimi si mtu wa maneno

UK 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 5**

**ACT WAZALENDO: CCM ISIHODHI MCHAKATO KUPATA KATIBA MPYA**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu amesema mchakato wa upatikanaji wa Tume Huru ya Uchaguzi na katiba mpya...

**UKURASA WA 5**

**BAJETI 2023/24**

**MAWAZIRI WACHUKUA HOJA SITA NYETI TOKA KWA WABUNGE**

MAWAZIRI wameahidi kufanyia kazi hoja sita za wabunge ikiwamo kupunguzwa tozo katika mawasiliano...





Wapiganaji wa Kundi la Mamluki la Wagner wakiwa mtaani katika jiji la Voronezh nchini Russia baada ya kuigeuka serikali ya nchi hiyo jana. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali yamulika wapotoshaji sakata la uendeshaji Bandari

UKURASA 2

# 'Bangi inayozalishwa Arusha ina kilevi kilichozidi viwango'

UK.3



**MICHEZO** **YANGA ILIVYOVUNA FAIDA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu ufafanuzi wa Mkataba ulioridhiwa na bunge wiki iliyopita kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai kwamba hakuna Bandari ya Dar es Salaam iliyouzwa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Samia: Mimi si mtu wa maneno

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema yeye si mtu wa maneno mengi, bali wa vitendo zaidi na hata watu wakisema, yeye anasonga mbele katika kuhakikisha maendeleo ya nchi yanapatikana.

Vilevile, amesema serikali inaendelea kufungua njia kwa ajili ya sekta binafsi na inajipanga vyema katika sekta za kilimo, mifugo na biashara kuhakikisha vijana wanapata ajira ili kujikwamua kiuchumi.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana aliposimama eneo la Soko la Tengeru na kusalimiana na wananchi wa Wilaya ya Arumeru na viunga vyake, alipokuwa anatoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

"Mimi si mtu wa maneno mengi, bali wa vitendo zaidi. Hivyo, hata watu wakisema, mimi ninasonga mbele na ninafanya hivi ili kuhakikisha maendeleo ya nchi hii yanapatikana. Kuna mambo mengi ya kufanya kwa vijana wa bajaj, bodaboda na makundi mengine," alisema.

Rais Samia alisema serikali imejipanga kikamilifu kuwezesha vijana katika sekta mbalimbali kupata ajira huku akiahidi kufungua fursa kwa sekta binafsi, hasa kwa vijana wanoendesha bodaboda, bajaj, wafugaji na wakulima.

Alisema anataka kuona uchumi wa vijana unaimarika kwa ustawi wa maisha yao na familia zao na kusisitiza vijana wa vyuo vya kati watapatiwa mikopo na serikali ili wasome bila hofu ya kukosa ada na mahitaji mengine muhimu chuoni.

Kuhusu ujenzi wa soko la kisasa la Tengeru, Rais Samia alisema serikali inatafuta fedha zaidi kwa ajili ya mradi huo. Kimekuwa kilio cha muda mrefu kutokana na miundombinu ya sasa kuwa chakavu.

"Ninajua changamoto kubwa inayowakabili wananchi wa Wilaya ya Arumeru ni soko la kisasa kutokana na soko lililopo miundombinu yake kuwa chakavu. Na sisi tuliahidi na hatujatekeleza.

"Ninataka niwahakikishie kuwa nitawajengea soko zuri ili mfanye biashara zenu katika mazingira rafiki," alisema.

Kwa waendesha bodaboda na machinga, Rais Samia alisema serikali ina kazi kubwa ya kufanya kwa ajili ya kuweka mazingira rafiki katika kufanya kazi zao za kila siku.

Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, alisema anamshukuru Rais Samia kwa ahadi ya ujenzi wa soko hilo ambalo ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa jimbo hilo.

Alisema soko hilo linakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu, hali ambayo inasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara hasa kipindi cha mvua.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alimshukuru Rais Samia kwa serikali yake kutoa fedha za miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema Mkoa wa Arusha umepata fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari.

# Serikali yamulika wapotoshaji wa sakata la uendelezaji wa Bandari

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema kumekuwa na upotoshaji mkubwa kuhusu makubaliano yaliyoingiwa baina yake na Dubai kuhusu uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, katika ufafanuzi wake kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema upotoshaji upo katika masuala mengi, ikiwamo hoja kwamba ni mkataba usiovunjwa.

Alisema serikali haiwezi kuridhia mkataba wa aina hiyo - usiokuwa na vipengele vya kuuvunja.

Alisisitiza kuwa endapo kuna upande ambao haujaridhia, mkataba huo unaweza kuvunjwa.

Msigwa alisema makubaliano yaliyoingiwa hayahusishi bandari zote kama baadhi ya aliowaita wapotoshaji wanavyoeleza.

"Makubaliano yaliyoingiwa ni ya ushirikiano na baada ya hapo wataeleza wanakwenda kushirikiana katika maeneo yapi na bahati nzuri makubaliano hayo yameitaja Bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Pia alisema makubaliano hayo yametoa nafasi endapo wakiona mwekezaji huyo anafaa wanaweza kumpatia maeneo mengine.

"Hivyo, unaweza kumpatia ama usimpatie. Kumekuwa na upotoshaji mwingi kwenye jamii kilichosainiwa mpaka sasa ni makubaliano ya ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai kwa ajili ya kupata manufaa katika uendeshaji," alisema.

Msigwa alisema maneno ya upotoshaji yamekuwa mengi na kukanusha madai kwamba bandari inakwenda kuuzwa.

"Sio kweli kwamba kupitia mkataba huo bandari zinauzwa, mara wengine wanasema miaka 100, mara mikataba isiyofutika. Maneno yamekuwa mengi, watanzania ondoeni hofu, kilichofanyika ni makubaliano baada ya hapo itakuja mikataba ya utekelezaji ya ile miradi ambayo itatekelezwa.

"Kwenye makubalaino hayo inaelekeza tutaanza kushirikiana katika uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam na siyo gati zote zimetajwa kwenye mkataba huu. Mpaka sasa bado hatujafanya mazungumzo ya awali, tulisema tutashirikiana chini ya wataalamu wetu kuingia katika majadiliano ya kina," alisema.

Alisema mkataba huo utawekwa wazi na hauwezi kuonyeshwa ukomo kwa sababu wapo katika majadiliano na kuwataka watanzania kutokuwa na hofu.

Alisema Rais Samia aliona kuna haja ya kuboresha bandari ili iwe na ufanisi wa kutosha na kuondokana na ukusanyaji wa mapato kidogo.

"Bandari yetu ya Dar es Salaam ina fursa kubwa ya kuhudumia nchi takribani nane zinazotuzunguka zisizokuwa na bandari lakini mapato tunayoyapata ni madogo na mapato ya forodha tunayopata ni Sh. trilioni 7.7.

"Wataalamu wanasema tukiwekeza tunaweza kupata Sh. trilioni 26.7, hizi ni fedha nyingi,"alisema Msigwa.

Akizungumzia miradi, Msigwa alisema uboreshaji wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka unaendelea vizuri huku ule wa Soko Kuu la Kariakoo ukitarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu na watu kufanya biashara saa 24.

# Serikali yatoa tahadhari ukame mkali maeneo mengi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amewataka Watanzania kutunza mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi unaotishia uhai wa viumbe hai kutokana na ukame mkali uliopo maeneo mengi ya nchi.

Dk. Jafo aliyasema hayo jana baada ya kushiriki upatandaji miti ulioandaliwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya kanisa hilo.

Alisema hivi sasa dunia imekumbwa na athari kubwa za kimazingira ambazo zinatokana na mabadiliko tabianchi, hali ambayo kila mtu anapaswa kutimiza wajibu wake katika kutunza na kuhifadhi mazingira.

"Huu ni mwezi Juni, ni muda mfupi sana tangu kuisha kwa mvua za masika lakini ukitembea katika maeneo mengi ya nchi, yana ukame kwelikweli, hii inaonyesha kuwa hadi itakapofika mwezi Novemba, hali itakuwa mbaya sana," alitoa angalizo.

Dk. Jafo alisema mabadiliko ya tabianchi yameathiri maeneo mengi ikiwamo kukauka kwa vyanzo vya maji, hali ambayo inatishia uhai wa mifugo na viumbe vingine.

"Hivi sasa athari za kimazingira zimeathiri hata bahari, kina cha maji kinaongezeka, nemba Pemba, nenda Unguja kuna maeneo ambayo yalikuwa makavu hivi sasa maji yanaongezeka.

"Hii yote ni kutokana na kuongezeka kwa joto duniani, barafu zinayeyuka hivyo, hali hii inatulazimu kuhakikisha kila mtu anatunza mazingira kwa nguvu zake zote," alisisitiza.

Waziri huyo alisema athari nyingine ya kimazingira ni kushuka kwa kiasi cha mvua na kusababisha kupungua kwa kiwango cha mavuno na kuchangia ongezeko la bei za vyakula.

"Wakati kama huu miaka ya nyuma, kilo ya mchele ilikuwa inauzwa kwa bei juu kabisa ilikuwa Sh. 1,800 lakini hivi sasa, imependa hadi Sh. 3,700 na tusione ajabu kuwa bei hii ikaendelea kupanda zaidi ya hapa," alisema.

Askofu wa KKKT Dayoyosi ya Dodoma, Christian Ndosa, alisema lengo la upandaji miti ni kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko tabianchi.

Askofu Ndosa alisema katika maadhimisho ya miaka 60 ya kanisa mwaka huu, wamepanga kupatanda miti 30,000 na wameanza na miti 1,000.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Maji na Mazingira, Anna Lupembe, alitoa wito kwa makanisa kuunga mkono jitihada za serikali za kupanda miti katika maeneo yao yote ya wazi.

# Waziri asema Bangi ya Arusha ina kiwango kikubwa cha kilevi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (pichani), amesema bangi inayozalishwa mkoani Arusha na mikoa mingine ina kiwango kikubwa cha kilevi kinachoharibu afya ya akili kwa watumiaji.

Jenista aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa matembezi ya hisani kuelekea kilele cha maadhimisho ya Kupinga Dawa ya Kulevya yanayotarajiwa kuhitimishwa leo na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa mujibu wa Jenista, bangi imekuwa inaharibu akili za watumiaji na kuchochea matatizo ya afya ya akili hususani kwa vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa.

"Bangi inayozalishwa huku Arusha eneo la Kisimiri Juu wilayani Arumeru mkoani Arusha ni hatari sana kwa afya ya binadamu kwa sababu inaharibu afya ya akili kwa vijana sanjari na watumiaji wengine huku Taifa likipata hasara kubwa ya kupoteza nguvu kazi ya Taifa," alisema.

Waziri Jenista alipongeza operesheni inayofanywa na Mamlaka ya Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA) ambayo hivi karibuni walikamata magunia zaidi ya 5,000 ya bangi mbichi wilayani Arumeru.

Katika hatua nyingine, waziri huyo alikagua maonyesho ya wadau wanaoshirikiana na serikali katika kupinga dawa za kulevya na kutoa huduma kwa waraibu wanaotokana na dawa hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema kwa sasa janga la uraibu ni kubwa kwa vijana kutokana na kujiunga katika makundi yasiyo rafiki ndani ya jamii. Alikitaja ni matendo ambayo tishio kwa taifa na kizazi kijacho.

"Niwasihi vijana kutumia fursa hii katika kupata elimu na kujiepusha na utumiaji wa dawa za kulevya, athari za utumiaji dawa za kulevya ni kubwa na inasababisha vitendo vya uvunjifu wa amani.

"Kipindi cha uongozi huu wa Rais Samia, serikali imejitahidi kuongeza vituo vya kutoa tiba kwa waraibu na kuwarudisha kuwa sehemu ya jamii na kuwa wajasiriamali na kuendelea kuwa tegemeo kwa familia zao," alisema.



Mongella aliiomba jamii iendelee kuwasaidia waathirika na kuacha kuwanyanyapaa kwa kuwa hawapaswi kutengwa.

Kamishna Jenarali wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema wataendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na vyombo vingine vya umma katika kuhamasisha wananchi kulima mazao mengine ya chakula na biashara, badala ya kuendeleza kilimo cha bangi ambacho hakina tija kwao na Taifa.


## KUPOTEA KWA CHETI



**KHALID NICKSON DAUD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5497/0114/2020** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NYIJUNDU SECONDARY SCHOOL** mwaka **2020.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chocote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/KIG/RB/213040/2023**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Temeke
Kituo cha Jumuishi
Mkoa D'salaam
Usimamizi wa mirathi Na. 929/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU
MASHAVU OMARY KIRUNDU
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA
MSIMAMIZI YALIYOLETWA
na RAMADHANI SADIKI KIRUNDU

**TANGAZO**
(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 mwezi 07 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 23 mwezi 06 mwaka 2023



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

# Wasiowajibika Wizara Kilimo kupelekwa kusoma magazeti

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema ugumu uliopo katika mfumo wa kuwafukuza kazi watumishi wa umma ndiyo chanzo cha wengi wao kufanya kazi kimazoea na kushindwa kuwajibika ipasavyo kuisaidia serikali kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Amesema atakachofanya kwa watakaoshindwa kutekeleza majukumu, ni kuwapeleka jengo lililopo karibu na Bunge ambako watakuwa wanasoma magazeti na kama serikali itaendelea kuwalipa mishahara, iendelee.

Bashe alitoa kauli hiyo juzi jijini humo alipokuwa akihutubia wajumbe wa mkutano wa 13 wa wadau wa kahawa uliofanyika kwa siku mbili.

Alisema moja ya sababu za serikali kushindwa kufikia azma yake ni watumishi wake kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Hadi umfukuze kazi mtumishi wa umma ni kazi sana, kuna mlolongo mrefu sana, na mimi sina uwezo huo sijapewa mamlaka hayo, ila mimi nitakachofanya kwa mtu yeyote ambaye nitaona anashindwa kutekeleza majukumu yake, kuna jengo lipo pale Fifty Six, nitawapeleka waende kusoma magazeti. Kama serikali itaendelea kuwalipa mishahara, iendelee kuwalipa," alisema.

Bashe alisema inashangaza kuona mtumishi wa umma anaingia kazini saa mbili asubuhi na kuondoka saa tisa alasiri bila kujali kama amekamilisha kazi zake wakati mkurugenzi wake anakaa ofisi hadi saa tatu usiku.

Kutokana na hali hiyo, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuwaondoa maofisa kilimo wote waliopo mjini na kuwapeleka vijijini.

"Inabidi waondoeni wote waende vijijini kama ambavyo walivyo walimu, leo hii tumegawa pikipiki lakini bado tunaziona mjini hadi wakati mwingine tunatamani hata tuzikusanye zile pikipiki zetu,"alisema.

Bashe pia alipongeza Bodi ya Kahawa kwa kufanikisha kuongeza mavuno ya zao la kahawa kwa mwaka hadi kufikia tani 45,000 ikiwa ni kiasi kikubwa kufikiwa tangu Tanzania kupata uhuru.

Alisema ili kuendelea kuimarisha zao hilo, serikali imepanga kuja na mkakati wa kuhamasisha matumizi ya kahawa ya ndani ili kuwa na uhakika wa soko.

"Nchi ya Ethiopia ambao ndiyo wanaongoza kwa uzalishaji wa zao hili Afrika, kinachowasaidia ni matumizi ya ndani. Sisi tunapanga kuhamasisha matumzi ya ndani ili hata soko la nje likiyumba tutaendelea kuwa na uhakika wa kuuza kahawa yetu," alisema.

Alisema tayari wameshaandika barua kwa vyuo vikuu 15 na viwili kati ya yake vimejibu na kutoa ruhusa ya kuanzisha migahawa ambayo itakuwa inahamasisha matumizi yake vyuoni.

"Kusafirisha kilo moja ya kahawa nje ya nchini ni takribani dola nne lakini kuingiza kilo moja ya kahawa ambayo tayari imeongozwa thamani ni dola takriban 20, hivyo ipo haja na kuwa na soko la uhakika la ndani kwanza," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa (TCB), Primus Kimaryo, alisema zao hilo linazidi kuimarika kila siku kutokana na uwezeshaji mkubwa wanaoupata toka serikalini na kwa wadau wa zao hilo.

Alisema kutokana na mikakati iliyowekwa na bodi hiyo, wanatarajia kufikia uzalishaji wa tani 300,000 wa zao hilo katika msimu wa kilimo wa 2025/26 na kuongeza uzalishaji wa miche milioni 20 ya kahawa kwa mwaka ili kufikia mahitaji ya wakulima.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TaCRI), Deusdededit Kilambo, alisema kuna kazi ya kufanya ili Tanzania iingie katika ushindani Afrika na nje ya bara hilo.

# Mpango: Viribatumbo, uzito mkubwa changamoto mijini

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema watanzania wengi, hususan wanaoishi mijini, wanakabiliwa na hali ya uzito uliozidi na viribatumbo, hivyo kupoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Amesema magonjwa hayo kwa kiasi kikubwa husababishwa na mtindo wa maisha, ulaji usiofaa na kutofanya mazoezi.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijiji Dodoma alipozungumza na wabunge na watumishi wa Bunge baada ya kumalizika kwa Tamasha la Bunge Grand Bonanza lililofanyika katika Shule ya Sekondari John Merlin. Alisema ni muda mwafaka wa kupinga kwa nguvu zote 'tabiabwete' ili kujikinga na magonjwa hayo kwa kujenga tabia ya kufanya mazoezi mara kwa mara.

Makamu wa Rais pia alitoa wito kwa Bunge kufanya semina au mjadala utakaolenga kuibua mapendekezo na mikakati mipya ikiwamo aina za uwekezaji endelevu, kutambua na kulea vipaji vitakavyowezesha michezo ambayo Tanzania inaipa kipaumbele ili kushinda katika mashindano ya kikanda na kimataifa katika kipindi kifupi," alisema.

Aliwahimiza wabunge kwa umoja wao kuwa mstari wa mbele kuhamasisha na kulea timu za michezo katika mikoa au majimbo hususani timu za wanawake, vijana wa shule za msingi na sekondari na watu wenye ulemavu.

Pia aliagiza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo yalindwe na kutobadilishwa matumizi, akisisitiza Bunge na serikali wawe mstari wa mbele kuhakikisha kuna ulinzi wa maeneo hayo.

Alisema ulinzi wa maeneo ya michezo unapaswa kwenda sambamba na uhifadhi wa mazingira kwa kupanda miti kuzunguka viwanja vya michezo, ili kuhakikisha upatikanaji wa hewa safi wakati wananchi wanafanya mazoezi au kushiriki mashindano mbalimbali.

Dk. Mpango alisema hivi sasa michezo imebainika kuwa na nafasi kubwa katika kukuza uchumi duniani kote ambapo ujenzi wa miundombinu ya michezo, kushamiri kwa sekta ndogo ya burudani na uzalishaji wa vifaa vya michezo ni chanzo kikubwa cha ajira na mapato. Bonanza hilo lihudhuriwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wawakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Pia walikuwapo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na wawakilishi wa benki hiyo pamoja na watumishi wa Bunge.

Tamasha hilo limefanyika kwa ushirikiano na Benki ya CRDB, likiwa na kaulimbiu ya "Tupende Michezo, Tujenge Taifa letu".



Kaimu Mwenyekiti, Eric Kitali ambaye ni Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) akiongoza kikao cha Kamati ya ufundi ya Serikali Mtandao kilichofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamera za usalama kufungwa shuleni kukabili ukatili kijinsia

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SHULE za umma na binafsi zimeagizwa kuangalia uwezekano wa kuweka kamera za usalama (CCTV) ili kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto shuleni.

Agizo hilo linakuja huku takwimu za kipindi cha miezi mitano kilichoanzia Januari mwaka huu, zinaonyesha kuwapo matukio 1,534 ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa kwa vituo vya kutolea huduma za afya kupitia Mfumo wa Takwimu za Afya (DHIS2).

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alitoa agizo hilo alipozungumza kwenye kikao kazi cha wadau wa elimu cha kuweka mikakati ya mkoa kuwalinda watoto shuleni dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Dk. Mganga aliziagiza shule za serikali na za binafsi mkoani humo kuangalia uwezekano wa kuweka kamera za usalama CCTV ili kukomesha vitendo vya ukatili kwa watoto.

"Matumizi ya teknolojia za kamera za usalama katika shule zetu zikiwekwa katika kila kona na katika magari ya kuwabeba wanafunzi, zitasaidia kuonyesha vitendo hivyo na kupata ushahidi wa moja kwa moja na kutokomeza ukatili wa aina zote hasa kwa watoto," alisema.

Dk. Mganga aliomba kuanzishwa kwa madawati ya ulinzi na usalama kwa mtoto shuleni, jambo litakalowafanya kuondoa woga wa kutoa taarifa za ukatili.

"Niwaagize maofisa elimu wote kuhakikisha shule zote zinakuwa na madawati ya ulinzi na usalama ili watoto wajadili masuala ya ukatili na kutoa taarifa," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imewekeza katika miundombinu ya elimu ili kumsaidia mtoto wa kitanzania kupata elimu bure na bora, hivyo ni jukumu la watendaji kusimamia watoto wasifanyiwe vitendo hivyo vya udhalilishaji.

Dk. Mganga alitoa rai kwa viongozi wa sekta ya elimu mkoani humo katika shule za msingi na sekondari watoto wafundishwe kupitia wimbo wa 'Don't Touch, kampeni iliyoasisiwa na Mkaguzi wa Polisi, Francis Msuku wa Kata ya Gambushi, Bariadi mkoani Simiyu.

"Ili kukabiliana na vitendo hivyo, aliwataka maofisa ustawi na maendeleo ya jamii kutoka ofisini na kwenda kwa wananchi kutoa elimu kuhusu haki na wajibu wao katika kumlinda mtoto na kuwaelekeza vizuri ni wapi pa kukimbilia ili kupata huduma zinazostahili.

Pia aliagiza urasimu katika utoaji huduma uondolewe kabisa ili kuleta imani kwa wananchi kuhusu vyombo vyao vya dola.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Victorina Ludovick, alisema katika kipindi hicho, matukio 670 ya ukatili wa kijinsia kwa watoto yametokea na kudhihirisha tatizo hilo bado ni kubwa mkoani hapa.

## HABARI KITAIFA



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akigawa injini ya boti kwa baadhi wakilishi wa vikundi vya uvuvi wa samaki na mazao bahari kwenye msimu wa pili wa Tamasha la Vyakula vya Baharini (Zanzibar Seafood Festival 2023) lililofanyika katika ufukwe wa Kendwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**

BAJETI 2023/24

# Mawaziri wachukua hoja sita kutoka kwa wabunge

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

MAWAZIRI wameahidi kufanyia kazi hoja sita za wabunge ikiwamo kupunguzwa tozo katika mawasiliano, kupunguzwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika mazao ya kilimo yanayozalishwa ndani na tozo katika mafuta na ngano.

Nyingine ni kuboreshwa miundombinu ya elimu, kusambazwa wa vifaa tiba vya afya, maboresho ya miundombinu ya barabara na kilimo na changamoto ya wanyamapori wakali hasa tembo kuvamia makazi ya watu na kuharibu mali.

Walitangaza kuchukua hatua hizo juzi walipochangia bungeni jijini hapa mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2023/24.

Katika mjadala huo, wabunge waliitaka serikali kuangalia namna ya kupunguza kodi katika mawasiliano ikiwamo katika miamala ya simu kwa kuwa zimekuwa mzigo mkubwa kwa mwananchi.

Wabunge pia waliishauri serikali kuongeza madarasa ili wanafunzi wote wanaofaulu hasa kidato cha tano wapate shule na kuhakikisha vyuo vya kati vyote vinaondolewa ada ili kuongeza wataalamu nchini.

Akijibu hoja kuhusu tozo mafuta na ngano, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wamekubaliana na Wizara ya Fedha na Mipango kupanga mikakati ya kuweka kodi ambazo zitakwenda kumlinda mkulima wa ndani.

Alisema serikali inaendelea kuweka fedha kwa ajili ya kugawa mbegu za kisasa za ruzuku pamoja na kuwa na teknolojia ya kisasa kwenye mashamba yanayozalisha mbegu. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alisema kupitia bajeti hiyo, watauongezea Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) fungu kufikia Sh. trilioni 1.235 ili kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara.

Pia alisema watatumia zaidi ya Sh. bilioni 248.5 kwa ajili ya kuongeza miundombinu ya elimu ili kuwapo shule za kutosha katika kidato cha tano na cha sita. Sh. bilioni 116 .92 zitasambaza vifaa tiba katika hospitali zaidi ya 31, vituo vya afya 278 na zahanati 367.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema bajeti hiyo kama ikipita itatekeleza ujenzi wa kampasi za vyuo vikuu 14 katika mikoa mbalimbali ikiwamo Singida, Tabora na Tanga na ujenzi wa vyuo vya ufundi katika wilaya 64 na chuo cha VETA Mkoa wa Songwe.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema serikali itapunguza gharama za mawasiliano na uendeshaji wa teknolojia, ikiwamo pendekezo la bajeti kupunguza gharama za kupitishia miundombinu ya mawasiliano barabarani kutoka dola 1,000 hadi kufikia dola 100 kwa kilomita moja kwa mwaka.

Alisema pendekezo la kutengwa fedha kwa ajili ya kufikisha umeme hadi kwenye vitongoji kwa kuwa litasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa minara kwa mafuta ya dizeli ambazo ni Sh. milioni 1.8 wakati ukitumia umeme ni Sh. 400,000. Nape alisema ni matumaini yake kuwa serikali itaendelea kupunguza kodi katika sekta hiyo hasa ya huduma za mawasiliano ambapo katika kila Sh. 100 inayolipwa Sh. 41 inakwenda kwenye kodi.NWaziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, alisema wanachukua hatua za haraka kutatua changamoto ya wanyama wakali ikiwamo tatizo la tembo lililolalamikiwa na wabunge wengi kabla halijawa kubwa zaidi.

Alimwomba Waziri wa fedha kuendelea kuwasaidia kifedha ili ziwasaidie kutatua changamoto nyingi zinazoikabili wizara hiyo ili kuongeza mapato ya ndani na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Exaud Kigahe, alisema wanaendelea kupunguza tozo katika sekta muhimu ikiwamo kilimo, afya, mifugo, utalii na taasisi za udhibiti na kuboresha mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambao wabunge wengi wameulalamikia.

Alisema wataaanzisha vitengo katika halmashauri ambavyo vitashughulikia masuala ya uwekezaji, viwanda na biashara ili kuwapunguzia mzigo watu kwenda wizarani kufuata huduma hizo.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Msongwe, aliwahakikishia kuunganisha mikoa kwa barabara za lami ikiwamo Kigoma na Katavi ambayo ilikuwa haijaunganishwa na huduma hiyo.

Kuhusu mabasi kusafirisha abiria kwa saa 24, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete alisema wanendelea kuboresha miundombinu ya barabara za kawaida na reli ili kuboresha miundombnu yake.

# Kambi ya wanafunzi yafunguliwa Zhejiang

**Na Mwandishi Wetu**

HAFLA ya ufunguzi wa kambi ya majira ya joto ya wanafunzi wa Sekondari na Taasisi ya Confucius ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ilifanyika Juni 19 katika Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang, China.

Wanafunzi na walimu 20 kutoka Tanzania walishiriki katika kambi hiyo iliyoandaliwa na Kitivo cha Kimataifa cha Utamaduni na Maendeleo ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Wang Hui, aliwakaribisha wageni hao kutoka Tanzania, na kuitakia mafanikio shughuli hiyo huku Mwalimu wa Tanzania anayeongoza msafara huo, Goodness Mfanga akishukuu Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang kwa maandalizi mazuri ya shughuli hiyo, na kueleza matarajio yake kwa shughuli zijazo katika kambi hiyo.

Siku hiyo, wanafunzi kutoka Tanzania walitembelea maktaba, makumbusho ya historia ya Chuo Kikuu na Jumba la Makumbusho la Afrika, ambako si tu walifahamu utamaduni wa nchi mbalimbali za Afrika, bali pia walijionea historia na hali ya sasa ya urafiki na mawasiliano kati ya China na Afrika.

Katika wiki mbili zijazo, wanafunzi hao watashiriki shughuli mbalimbali ikiwamo kujifunza lugha ya Kichina, kutembelea miji ya China na kujionea urithi wa utamaduni wa China, ili kuimarisha uelewa wao kuhusu lugha, utamaduni na jamii ya China.

# ACT Wazalendo: CCM isihodhi mchakato kupata katiba mpya

**Na Mwandishi Wetu,** URAMBO

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu amesema mchakato wa upatikanaji wa Tume Huru ya Uchaguzi na katiba mpya unapaswa kuwa shirikishi, wazi na jumuishi.

Ado alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti juzi katika mikutano ya majimbo ya Kaliua na Urambo mkoani Tabora.

"Nimemsikia Katibu Mkuu wa CCM, Ndugu Daniel Chongolo, akisema mchakato wa kuandikwa wa katiba mpya utasimamiwa na kuratibiwa na CCM.

"Hatutokubali hilo litokee. Hii si katiba ya CCM, ni katiba ya Watanzania. Inapaswa kupatikana kwa mchakato wa wazi, jumuishi na shirikishi kwa makundi yote katika jamii.

"Ni muhimu tujifunze kilichokwamisha mchakato wa katiba mpya mwaka 2014. Somo la kwanza ni kutanguliza mbele maslahi ya vyama dhidi ya maslahi ya Taifa.

"Ni muhimu vyama vyote vya siasa na makundi yote muhimu katika jamii yashirikishwe katika kujenga mwafaka wa kitaifa ili tusikwame tena," alisisitiza Ado.

Katibu Mkuu alirejea rai ya ACT-Wazalendo ya kuandikwa upya kwa Sheria ya Uchaguzi ndani ya mwaka huu ili kuanzisha Tume Huru ya Uchaguzi itayosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu ujao. Pia, Ndugu Ado ameitaka Serikali mwakani na iweke wazi lini mchakato wa katiba mpya utaanza.

Alisema ni hatua muhimu za kupitiwa upya kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya kura ya maoni; kuitishwa kwa mkutano wa majadiliano ya kitaifa kuhusu katiba na kuundwa kwa kamati ya wataalami ya kuchambua maoni ya wadau na kuandika katiba pendekezwa itayopigiwa kura ya maoni.

Baada ya ziara yake katika mikoa ya Kigoma na Tabora, Katibu Mkuu anatarajiwa kuingia Tanga leo na atakuwa na mikutano hadi Juni 28 mwaka huu.

Kwa mujibu wa Janeth Rithe, Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma ACT Wazalendo, katika ziara yake hiyo mkoani Tanga, Ado atazungumza na viongozi wa kata zote za majimbo ya Tanga Mjini, Pangani na Mkinga kupitia mikutano mikuu ya majimbo hayo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuwe na mkakati kuukabili ukame unaogonga hodi nchini

**SERIKALI** jana ilitangaza kuwapo dalili za nchi kukumbwa na ukame mkali mwishoni mwa mwaka. Shida kuu ni kilio cha ulimwengu mzima-mabadiliko ya tabianchi.

Ni hadhari iliyotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo. Rai yake kwa Watanzania ni kutunza mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko hayo yanayotishia uhai wa viumbe hai.

Waziri huyo alifafanua kuwa katika kutekeleza majukumu yake, amebaini kwamba hadi sasa, ikiwa ni muda mfupi baada ya kumalizika kwa msimu wa kilimo kwa wanaotegemea mvua, kuna maeneo mengi nchini yameanza kukumbwa na ukame.

Alikitaja ni kiashiria kwamba kufikia mwezi Novemba, hali itakuwa mbaya.

Akahimiza wananchi kuwa na hadhari, wazidi kupanda miti kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Nipashe Jumapili tunakumbusha kwamba ukame huathiri wanaotegemea maji kupitia mito, visima na mabwawa na husababisha ukosefu wa maji safi na salama, pia chakula.

Mifugo huathirika kwa kukosa malisho na maji, hivyo wafugaji hulazimika kuhama.

Ni kipindi ambacho mifugo mingi hufa kutokana na kukosa malisho na maji.

Athari za ukame zinaigusa pia sekta ya uhifadhi wa wanyamapori. Mbugani majani hukauka, upatikanaji wa maji huwa wa uhakika kwa wanyamapori wachache wenye uwezo wa kuvamia makazi ya watu. Hapo huibuka mgongano kati ya binadamu na wanyamapori.

Hadhari hii ya ukame mkali unaobisha hodi, itusukume kutunza chakula na kuwa na matumizi endelevu ya vyanzo vya maji vilivyopo.

Nipashe pia tunasisitiza serikali ichukue hatua kwa kuhakikisha Taifa lina akiba ya kutosha ya chakula. Pia kuwapo mkakati mahususi wa kuwanusuru wananchi dhidi ya shida hiyo.

Tunakumbusha kuwa mwishoni mwa mwaka jana, maeneo mengi nchini yalikumbwa na ukame.

Wilaya ya Monduli mkoani Arusha iliathirika zaidi, wakazi wake walipolazimika kuweka majivu katika tope ili wapate maji ya kunywa, hata serikali ikafikia hatua ya kugawa ndoo moja ya maji kwa kila kaya kwa siku.

Kimsingi, kilichoshuhudiwa wilayani Monduli kiliyakumba maeneo mengi nchini kutokana na ukame, japo maeneo mengine hayakufikia hatua ya serikali kugawa ndoo ya maji kwa kila kaya.

Maeneo mengi nchini mwishoni mwa mwaka jana kuliripotiwa mifugo kukosa malisho na maji huku baadhi ya halmashauri zikilazimika kupatiwa chakula cha dharura kutokana na upungufu wa chakula.

Si hayo tu, Oktoba mwaka jana kulikuwa na ripoti ya hali ngumu ya kimaisha iliyowakabili wakazi wa Mtera mkoani Dodoma kutokana na uhaba wa samaki kwenye Bwawa la Mtera linalotegemewa kiuchumi na wakazi wengi wa eneo hilo.

Kwa kuzingatia uzoefu huo wa mwaka jana pamoja na tahadhari ya jana ya Waziri Jafo, kuna haja kuchukua hatua kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuepuka vichocheo vyake ambavyo ni pamoja na uharibifu wa mazingira na matumizi ya nishati chafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii ishiriki vita dhidi ya mimba za wanafunzi

Na Sabato Kasika

**MIMBA** za utotoni ni tatizo sugu kwa wanafunzi, hasa katika shule za umma, ambao hurubuniwa na vijana wa mtaani, watu wazima na wakati mwingine walimu wao shuleni.

Tatizo hilo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mmomonyoko wa maadili kwa watoto kuanzia ngazi ya familia, wazazi na walezi wakiwa kiini cha uhalifu huo.

Ninaeleza hivyo kwa kuwa kumekuwapo na malalamiko wazazi wameshindwa kutoa malezi bora watoto wao tangu hatua ya awali na kusababisha wakose msingi bora wa maadili.

Pia lipo kundi katika jamii inayowazunguka watoto, lina tamaa ya uhusiano wa kingono na wanafunzi, likiamini wako salama, hawana maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

Baadhi ya wanafunzi wana tamaa ya kumiliki 'vitu vizuri', wanaingia katika mitego ya kundi ovu na kushiriki nalo ngono katika umri mdogo ili wapate fedha na kutimiza matamanio yao ya kupata 'vitu vizuri'.

Tamaa ya baadhi ya walimu kwa wanafunzi wao ni tatizo lingine linaloendelea kujitokeza na kusababisha kuwapo mimba za utotoni miongoni mwa wanafunzi. Wanaopaswa kuwa walezi kitaaluma kwa watoto, wanajitwisha majukumu ya baba - wa mtoto aliyebeba ujauzito na wa mtoto atakayezaliwa na mtoto mwenziwe.

Katika mazingira hayo, pia wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hutuhumiwa kushirikiana na wale wanaowapa watoto wao mimba kwa kupewa chochote na kumaliza kesi kimyakimya.

Yote hayo kama hayatochukuliwa hatua za kuyakomesha, ni dhahiri mimba hizo zitaendelea kuwapo na hivyo kukwamisha ndoto za wanafunzi, ingawa kwa sasa wameruhusiwa kurejea shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Je, wana ufanisi darasani? Kusoma huku unalea?

Ninafikiri umefika wakati sasa jamii kuhusika kikamilifu katika vita hii. Jamii ikemee na izungumzie madhara ya mimba hizo za utotoni kama njia mojawapo ya kusaidiana na serikali katika vita hiyo.

Hivyo, ni vyema sasa serikali ikaendelea kutoa adhabu kali kwa wale wanaobainika kuwapa mimba wanafunzi, lakini pia jamii iwe tayari kutoa ushirikiano kwa serikali, ili kusaidia kukomesha vitendo hivyo.

Ufuatiliaji wa karibu wa tatizo hilo ufanyike, ili kuzibana familia zenye mtindo wa kumalizana kimya kimya na wahalifu zisipate mwanya wa kuwaficha 'mafataki' kwa kupewa chochote.

Pamoja na hayo, ni vyema wanafunzi wapewa elimu kuhusu madhara ya uhusiano wa kingono wawapo shuleni, huku wazazi na walezi nao wakisimamia maadili mema kwa watoto wao.

Ikumbukwe kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 na 2022 wanafunzi 90,011 walipata ujauzito- shule za msingi wakiwa 1,554 na 7,457 wa sekondari. Hizi ni takwimu za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Ni takwimu zilizomshtua Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson, akiitaka wizara hiyo kuandaa takwimu kuhusu idadi ya wanaume walioshtakiwa na kupatikana na hatia ya kuwapa ujauzito wanafunzi.

Spika alilenga kuona kama sheria ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo hivyo inafanya kazi. Ninaamini wazazi na walezi wakikataa kupokea chochote na kumalizana na wahalifu ambao hutumia umaskini wa kipato wa baadhi ya familia kufanya vitendo hivyo, tutapunguza idadi ya mimba za aina hii.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Wanapigiaje kelele rasilimali bandari, lakini katiba, uhuru wao wako kimya



Pascal Mayalla

LEO ninaendelea na mada ya wiki iliyopita kuhusu makubaliano ya kiserikali, IGA ambapo Bunge letu limeridhia serikali yetu kuingia mkataba wa HGA na kampuni ya DPW ya Dubai, kutuendeshea Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Ni jambo zuri na jema kwa maslahi ya taifa, lakini bado kuna kelele nyingi huku na kule, kupinga jambo hii. Baadhi ya hoja za kupinga ni hoja za msingi na zina mashiko, ambazo inabidi serikali yetu izizingatie, lakini hoja zingine ni kelele tu kutokana na watu kutokujua.

Tatizo kubwa lipo hapo katika kutokujua, ukosefu wa elimu! Kwenye hili la Bandari, Watanzania wanahitaji kuelimishwa tu.

Hivi karibuni nimetembelea Idara ya Habari - MAELEZO. Nilikutana na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, ikiwa ni mara ya kwanza tangu ateuliwe.

Nikampongeza kwa uteuzi na kumshushia yeye zigo lote la lawama kwa hizi sintofahamu zote, zinazoendelea kuhusu hili la Bandari, kwa kumweleza limefikia hapa kwa kukosekana uwazi na elimu kwa umma kuhusu jambo hili.

Nikampongeza kwa kuanzisha ule utaratibu wa kuita viongozi na kutolea ufafanuzi mambo ya msingi kule Club House, lakini hizo Club House ziwe za 'proactive' na sio kusubiri kelele ndipo wanakuja na ufafanuzi!

Tangu kelele za mkataba kuanza, kwanini mpaka sasa hakuna kipindi chochote cha elimu kwa umma kuhusu hili? Msigwa alimalizia kwa taarifa ya kutia moyo sana, Maelezo inakwenda kufungua studio yake.

Watanzania ni watu wa ajabu sana! Wanapigaje kelele kwa mkataba kamoja tu wa rasilimali bandari, lakini kuna mambo makubwa muhimu sana ya msingi kama shida zilizopo kikatiba na kuporwa kwa uhuru wao, ambayo ni mambo muhimu sana? Kwanini Watanzania wako kimya kwenye mambo makubwa ya msingi ya Katiba yao kuwa ya aina hii na uhuru wao kuporwa, halafu wanapigia kelele suala la rasilimali bandari?

Ili nisionekane na mimi ni mpinzani, ninamshauri Rais Samia usiwasikilize kabisa wanaopinga ukodishwaji wa bandari kwa kampuni ya DPW ya Dubai, kwa hoja mufilisi, wapuuzwe, wanaopinga kwa hoja za msingi, wasikilizwe ili kazi nzuri ya Rais Samia iendelee, ili HGA iwe safi na imenyooka!

Kati ya Katiba, uhuru na rasilimali, kipi ni muhimu zaidi? Kitu muhimu cha kwanza kwenye nchi yoyote ni watu, uhuru wao na Katiba yao, mengine yote ikiwamo rasilimali yanafuata.

Watanzania nimewaelezea kuwa ni watu wa ajabu sana kwa sababu katiba yao ina shida, lakini wamenyamaza kimya! Kwanini haki zao mbili kuu za msingi za kuchagua na kuchaguliwa zimeporwa na kufinyangwa finyangwa huku Watanzania wamenyamaza kimya tu, wanaangalia?

Serikali yao imetunga sheria batili kinyume cha katiba, ikazipeleka bungeni kutungwa kuwa sheria! Bunge lililosheheni wanasheria nguli, wabobezi na wabobevu baada ya kupokea muswada huo, likazipitisha sheria hizo batili kwa kuzitunga kuwa sheria! Watanzania wamenyamaza kimya tu, wanaangalia!

Rais wa JMT hajawahi kuwa mwanasheria, anawategemea wasaidizi wake wabobezi na wabobevu wa sheria, kama wamezipitisha, sheria hizo batili, akazisaini kuwa sheria kamili licha ya ubatili wake!

Mchungaji Mtikila (marehemu), alifungua shauri Mahakama Kuu kupinga sheria batili hiyo, bila sapoti ya Watanzania huku watanzania wengine wote wamenyamaza kimya tu, wanaangalia!

Mahakama Kuu, ikatamka sheria hizo ni batili zifutwe toka vitabu vya sheria! Serikali yetu ikakata rufani kupinga uamuzi huo wa Mahakama Kuu, ikashindwa!

Baada ya serikali kushindwa, ikapeleka bungeni mabadiliko ya katiba ya JMT kwa kuvichomekea vipengele hivyo batili, Bunge livichomekee kiubatili ndani ya katiba yetu! Yakafanya mabadiliko batili ya katiba yetu ya JMT na kuuchomekea ubatili huo ndani ya katiba yetu, huku Watanzania wakiwa kimya tu, wanaangalia!

Mchungaji Mtikila hakukubali Katiba yetu inajisiwe, kwa kuchomekewa ubatili! Akafungua shauri lingine kupinga mabadiliko hayo ya katiba kuingiza ubatili ndani ya katiba yetu.

Mahakama Kuu, ikampa ushindi Mchungaji Mtikila, ikatamka mabadiliko hayo ya katiba ni batili na yamechomekewa ndani ya katiba yetu kiubatili!

Serikali yetu makini yenye wanasheria nguli wabobezi na wabobevu, ikakata rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu iliyotimiza wajibu wake kikamilifu kupinga Katiba yetu kunajisiwa kwa kuchomekewa batili kiubatili!

Mpaka leo ninapoandika hapa, batili hiyo iliyochomekewa kiubatili ndani ya katiba yetu bado ipo! Ina maana tuna katiba yenye ubatili ndani yake!

Bado tuna sheria batili ndani ya sheria zetu, zinazopora uhuru wa Watanzania kuchagua na kuchaguliwa.

Unanyamaziaje Katiba na uhuru wako unaporwa, halafu unapigia kelele jambo la kheri kama uendeshaji wa Bandari?

**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# E-Mrejesho; dawa ya viongozi wasio na maadili



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WATOTO wanapozaliwa katika familia, ni matarajio ya wazazi kuwaona wakiwa si tu na afya njema, bali mwenendo na tabia njema, pia kuishi vyema na wenzao.

Hivyo wazazi hufurahi kuona watoto wanaishi katika mwenendo huo, lakini hiyo pia hutegemea na mwenendo wa maisha ya wazazi wao.

Endapo wazazi wakiwa na tabia mbaya, bila shaka watoto nao wataiga na kuwa na tabia kama hiyohiyo na hatimaye familia kuonekana haifai machoni mwa jamii.

Mwenendo na tabia njema, ndiyo nidhamu na wengine husema ndiyo maadili, hivyo maadili mema ni matamanio ya kila familia na kila jamii.

Familia na jamii zinapokuwa na tabia njema, maana yake hata Taifa zilimo familia na jamii husika, huonekana kuwa na maadili mema.

Katika ngazi za kitaifa, tumeshuhudia baadhi ya viongozi wakikosa maadili mema na hivyo kushindwa kuongoza watu wao na hatimaye kusababisha matukio hasi.

Baadhi ya viongozi kwa kukosa maadili, wamekuwa wanajihusisha na matendo ya ubadhirifu, dhuluma, wizi na ufisadi dhidi ya jamii wanazoziongoza na kuathiri mustakabali mwema wa Taifa.

Lakini kwa kubaini hayo, ndiyo sababu baadhi ya serikali huanzisha taasisi za kusimamia maadili mema kwa ajili ya viongozi wao na kurejesha imani kwa wanaowaongoza.

Tanzania ni moja ya mataifa yenye taasisi kama hizo, kwani katika ofisi ya Rais, kuna taasisi inayojulikana kama Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inayosimamia maadili na nidhamu kwa viongozi hao.

Taasisi hii ipo na imekuwapo tangu Julai 1996 lakini ni dhahiri si wengi wanaojua kuwapo kwake na majukumu yake kimsingi, katika kusimamia maadili ya viongozi wa umma.

Lakini kwa wanaofuatilia matukio na habari mbalimbali, wamekuwa wakiona hususan siku ambazo kiongozi mkuu wa nchi akiapisha wateule wake, kuna jaji husimama kuwalisha kiapo cha utii.

Jaji huyo ndiye kiongozi wa taasisi hiyo muhimu, ambaye kwa sasa ni Jaji Sivangilwa Mwangesi akimbulika kama Kamishina wa Maadili, na kwake viongozi hutoa matamko ya mali walizonazo.

Sekretarieti hiyo ndiyo hufuatilia tabia za viongozi wa umma na kudhibiti mgongano wa maslahi, ili kujenga imani kwa umma katika kukuza maendeleo ya Taifa.

Viongozi hao wana wajibu wa kutoa matamko kuhusu rasilimali, maslahi na madeni waliyonayo na kuchunguzwa endapo watakuwa wamekiuka maadili. Kimsingi, Sekretarieti ina dhima ya kuhakikisha kuwa kiongozi anakuwa mwadilifu ili kuwa mfano kwa anaowaongoza, akijiepusha kupokea rushwa na zawadi za thamani kubwa.

Kwa mujibu wa Sekretarieti, kiwango cha thamani ya juu cha zawadi anayopaswa kupokea kiongozi si zaidi ya Sh. 200,000 na endapo kitazidi hapo, atatakiwa kuisalimisha, ili ifanye kazi nyingine kwa mujibu wa sheria.

Mathalani, kiongozi husika amepewa zawadi ya gari, atatakiwa kulisalimisha ofisini ili litumiwe kwa manufaa ya wengi na si ya kwake na familia yake. Hayo ndiyo maadili.

Lakini ni wangapi hufanya hivyo? Wapo baadhi ya viongozi wanaomiliki mali lakini wakaziandikisha kwa majina ya ndugu na jamaa, ili isibainike, ingawa Sekretarieti kisheria ina mamlaka ya kuchunguza na kubaini hilo na kuchukua hatua.

Ndiyo sababu inamtaka kila mtanzania kusaidia kubaini maslahi fiche waliyonayo viongozi na kuyatolea taarifa kupitia mtandao ambao uko wazi na umetolewa na Sekretarieti kupitia mfumo au progranmu maalum ya kutolea taarifa.

Hiyo itasaidia kuwabaini viongozi wanaojificha nyuma ya ukwasi haramu na kufanya mambo kinyume cha maadili na kuichafua serikali lakini pia kutowatendea haki wananchi wanaoongozwa nao.

Kwa mujibu wa Jaji Mwangesi, yeyote mwenye taarifa kuhusu kiongozi anayekiuka maadili, basi akiingia katika mfumo, atakutana na programu ya e-Mrejesho ambayo hutuma, kupokea na kufuatilia malalamiko, mapendekezo, maulizo na pongezi.

Huko atakutana na majina ya taasisi za umma na kutuma anachotaka kukiweka katika mfumo huo na anachotaka kufanya kama ni kushtaki, kupongeza na kadhalika kama ilivyobainisha kwapo juu.

Ni ni njia nzuri ambayo haimweki hadharani mtoa taarifa, hivyo kubaki kuwa salama huku ikiisaidia Sekretarieti na Taifa kwa jumla, katika kuumbua viongozi wasio na uadilifu.

Atakuwa amewasiliana na taasisi zote vikiwamo vyama vya siasa na wizara zote. Hivyo Sekretarieti hii ni muhimu na inayostahili kusaidiwa, ili kutenda haki kwa wananchi viongozi na Taifa kwa jumla.

**Alamsiki!**

# WCF watoa msaada wa vifaa tiba Mwananyamala

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeikabidhi Hospitali ya Rufani Mwananyamala mkoani Dar es Salaam vifaa tiba mbalimbali ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi msaada huo jana, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano WCF, Laura Kunenge, alisema hospitali na watoa huduma za afya ni wadau muhimu na ni kiungo baina ya mfuko na waathirika wa magonjwa au ajali zinazotokana na kazi.

Alisema WCF katika kuadhimisha siku hiyo ambayo kufanyika kuanzia Juni 23 kila mwaka kwa lengo la kutambua mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo ya Bara la Afrika, wameona wawakumbuke wagonjwa.

"Jukumu kubwa la WCF ni kutoa fidia pale mfanyakazi anapoumia au kuugua kutokana na kazi. Msaada huo ni katika kutambua mchango wa watumishi wa umma katika kuhudumia wananchi. Mfuko unaamini msaada huo utarahisisha utendaji wao wa kazi na hivyo kuleta tija katika sekta ya afya.

"Watumishi ni sehemu ya umma na WCF ni sehemu ya umma kwa sababu inatoa fidia kwa wafanyakazi, na ninyi mnahudumia jamii."

Alisema wanaamini wakiwaunga mkono kwa kutoa vifaa zaidi, watumishi watatoa huduma zenye ubora zaidi na wagonjwa kupona na kurejea kwenye uzalishaji na kuendelea kulijenga taifa.

Laura alimpongeza Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha huduma za afya, kukishuhudiwa ongezeko kubwa la miundombinu ya afya katika maeneo mbalimbali nchini.

Katibu wa Hospitali ya Rufaa Mwananyamala, Lydia Nzema, aliishukuru WCF kwa msaada huo wa vifaa tiba ambapo alisema vitasaidia kuongeza tija katika kutoa huduma kwa wananchi.

"Hospitali hii inahudumia jamii yote iliyo katika eneo hili, na tunahudumia watu wengi, vifaa hivi vitarahisisha na kupanua wigo wa utoaji huduma," alisema.

Maofisa Wafawidhi wa WCF Kanda ya Kati, Nyanda za Juu Kusini na Kanda wa Ziwa walitoa wito kwa waajiri kujisajili kwenye mfuko ili kuwawezesha watumishi wao kuwa na uhakika wa kipato pindi wanapopatwa na majanga wawapo kazini.

"Tunapenda kuwakumbusha watumishi wa umma Tanzania Bara kuzingatia miongozo ya usalama na afya mahala pa kazi, lakini inapotokea bahati mbaya mtumishi amepata changamoto ya ajali kazini au ugonjwa afike ofisi za WCF ili aweze kupata haki zake kama mtumishi," alisema Nuru Ashraf, Ofisa Mfawidhi WCF Kanda ya Kati.

Ofisa Mfawidhi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rose Satta, alisema katika maadhimisho hayo wameendelea kutoa elimu na kuwahudumia waajiri na watumishi huku akitaka watumie huduma hiyo kutoa taarifa za matukio ya ajali, magonjwa au kifo ili madai yachakatwe kwa haraka.

# DC Temeke aagiza usafi kwenye maduka siku maalum

**Na Restuta James**

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Mwanahamisi Munkunda, ameagiza wafanyabiashara wa maduka yaliyo barabara kuu kufungua biashara saa 3:00 asubuhi katika siku maalum ya usafi.

Akizungumza jana na wakazi wa Kata ya Toangoma, Mwanahanisi alisema wananchi wote wanapaswa kushiriki kikamilifu siku ya usafi, hivyo wenye maduka ni sehemu ya hilo.

"Siku ya usafi tunafanya usafi kwanza halafu tunakwenda kufanya biashara, haina tija sana na wala haivutii wenzenu wanafanya usafi wewe unaendelea na biashara na unazalisha uchafu," alisema.

Mwanahamisi alisema jukumu la usafi wa mazingira ni la wakazi wote wa Temeke na kuwaomba kushirikiana ili kuing'arisha wilaya hiyo.

Meneja Mawasiliano wa Hospitali ya Alexia, Ali Mussa, iliyoratibu kampeni ya usafi wa mazingira katika Kata ya Toangoma, alisema wao ni wadau wa afya ya jamii, hivyo ni jukumu lao kushirikiana na wananchi katika kuimarisha sekta ya mazingira.

Alisema mbali ya kuimarisha usafi wa mazingira, hospitali hiyo imeboresha huduma zake kwa kutoa vocha maalum kwa wananchi wasio na bima ya matibabu, itakayowawezesha kutibiwa kwa gharama ndogo.

"Tumetengeneza kadi maalum inayotoa tiba nusu ya gharama, utapata huduma zote ndani ya hospitali kama wagonjwa wengine bila ubaguzi," alisema.

Alisema wametoa kadi hiyo ili wananchi wengi zaidi hasa wa kipato cha chini wapate matibabu kwa gharama ndogo.

Ali alisema hospitali hiyo inatoa huduma zote muhimu na za kibingwa zikiwamo za magonjwa ya wanawake, watoto, viungo, mifupa, meno na vipimo vya maabara, kwa wagonjwa wa nje na wa kulazwa.

Meneja wa Benki ya Equity, Tawi la Mbagala, Salum Khalfan, alisema wameshiriki kampeni ya usafi wa mazingira ili kusogeza huduma zao karibu na wananchi.



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Tuangoma Kata ya Tuangoma Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam, Mohamed Chande (kushoto), akiwaongoza wafanyakazi wa Hospitali ya Alexia iliyopo Tuangoma na wafanyakazi wa Benki ya Equity kufanya usafi katika Kata hiyo jana kulia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi wa hospitali hiyo, Hamis Muhagama. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtafiti ataka maboresho ya sera ya utafiti nchini

**Na Romana Mallya**

MTAFITI wa dawa za asili, Twalibu Msigwa, ameshauri sera inayohusiana na masuala ya utafiti, iboreshwe ili kutoa uwanja mpana kwa watafiti.

Amesema kuwa kwa sasa wanapofanya utafiti wa jambo, hata kama lina matokeo chanya, halifiki mbali kutokana na utaratibu uliopo sasa.

Msigwa ambaye ni mwasisi wa dawa ya asili ya 4A9, aliyasema hayo hivi karibuni mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kilio hicho, akibainisha kuwa tayari ameshawasilisha barua ya wazi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ili asaidie katika hilo.

Alisema amemwandikia barua ya wazi Rais Samia na tayari imeshawasilishwa ofisi kwake mwanzoni mwa wiki hii kumwomba awasaidie watafiti wanapofanya utafiti isiwe lazima mpaka upelekwe katika taasisi fulani. "Utafiti maana yake ni kutafuta, kila mtu ana utaratibu wake wa kutafuta, mradi njia anazotumia kutafuta ziwe sahihi na wazi na sahihi na zenye faida kwa taifa.

"Nimemwandikia barua ya wazi Rais kumjulisha jambo hili na leo (Jumatatu) asubuhi barua yangu imepokewa Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma. Hili ni jambo la kwanza nililowasilisha kwa Rais.

"Tunaomba waboreshe sera kusiwe ni taasisi fulani ndio iwe na uwezo wa kupitisha kitu, kuwe na utaratibu ambao utasaidia kukuza utafiti wetu kwa faida ya taifa," alisema.

Msigwa alitaja jambo la pili ambalo amemwomba Rais kulifanyia kazi ni ada za mchakato wa usajili na za vibali vya matangazo, ambazo kwa mwezi wamekuwa wakilipa Sh. 150,000 kwa tangazo moja, hivyo wanaomba liangaliwe ili kuwapunguzia mzigo.

"Faida ya kusajili dawa inabidi watanzania wajulishwe, kwa hiyo nimemwomba Rais atusaidie ili mtanzania aondolewe zile ada na kama kuna usumbufu wowote uondolewe ili kuwe na uhuru wa kueleza kile ambacho watanzania wanaweza kunufaika nacho kupitia kitu kilichofanyiwa utafiti na mtanzania mwenzao," alisema.

Jambo la tatu, alisema katika barua hiyo amemwonyesha kwa ushahidi vyeti saba mpaka 10 vinavyoonyesha namna mtu anaweza kutoka kwenye maambukizi na kuonekana hana maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

"Nimefanya hivyo ili aweze kushawishika kuona kwamba, kuna uwezekano tukiwawekea mazingira rafiki watafiti wanaweza kuja na suluhisho la changamoto ya taifa kuhusu masuala ya afya," alisema.

Alibainisha kuwa tayari serikali kupitia Wizara ya Afya imeshampatia kibali cha kuendesha kliniki kilichotolewa Desemba 8, 2022.

Alisema dawa ya asili ya 4A9 alianza kuifanyia kazi rasmi Julai 26, 2007, baada ya kupimwa na kuonekana ni salama kwa matumizi ya binadamu.

"Nilianza kuwapa watu wa eneo la Kibaoni, Ifakara, Mkoa wa Morogoro, na ilionyesha matokeo chanja kwa watu kupata unafuu. Nilipokusanya maoni vijiji vyote nilivyokuwa ninapita niliwasilisha wizarani na wizara ikanipongeza.

"Mheshimiwa Rais ninaomba kutumia fursa hii kuipongeza Wizara ya Afya kwa kuchukua hatua ya kusajili dawa na hadi leo ni dawa nyingi wamesajili na zinawasaidia," alisema.

# MAISHA

JUNI 25, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14



## VITUMBUA VYA NAZI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15





## HARUSI


Ukurasa 12




# FULANA INAPENDEZA

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| P | ■ | U | P | E | P | O |
| U | ■ | ■ | ■ | Z | ■ | N |
| N | ■ | A | L | E | ■ | D |
| G | U | U | ■ | K | O | O |
| U | ■ | N | A | E | ■ | S |
| Z | ■ | G | ■ | ■ | ■ | H |
| A | B | E | B | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


KOA, ARA, MTO, KAA, NYOKA, MAKAA, AGANO, ZUNGU, USHAMBA, MSHAMBA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

MALIZIA MCHORO HUU KWA KUUNGANISHA NUKTA KUTOKA NAMBA 1 MPAKA 20



## WATOTO

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

## CHEKA

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**

Paka ana manufaa gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Yatakayofanya mama mkwe akuchukie

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mtiririko wa mada iliyoanza wiki mbili zilizopita kuhusu ndoa, nikakazia mambo mke anapaswa kufahamu kuhusu wakwe. Pia nilieleza kinachowapata wanawake wanaodharau wakwe zao.

Ukienda katika sherehe za harusi, wakati wazazi wa maharusi wanatoa nasaha kwa vijana wao, binti huwa anaambiwa na wazazi wake;

Binti yangu, ninakutakia maisha mema katika ndoa yako. Mpende mumeo na elewa kwamba wazazi wake ni wazazi wako pia, uwaheshimu, uwapende na kuwatii...”

Yapo mambo mengi huwatamkia kwa lengo la kuimarisha ndoa yao. Lakini kinachotokea baadaye ni tofauti na maagizo hayo, hivyo kuleta mtikisiko mkubwa katika ndoa nyingi.

Kama nilivyoeleza wiki iliyopita, wanawake wengi wanashindwa kuishi katika ndoa zao kwa sababu ya kutoishi kwa akili na wakwe.

Kwa mfano, wanasahau kuwa mama mkwe hana tofauti na mama yake mzazi. Lakini anamfanyia mzaha na dharau, jambo ambalo huamsha hasira na kuamua kile anachoweza kufanya.

Leo msomaji wangu nikupitishe katika baadhi ya sababu zinazomsukuma mama mkwe kukuchukia. Wivu ni moja ya sababu. Fahamu kuwa baadhi ya mama wakwe hawafurahii kile ambacho wake wa vijana wao wanafurahia.

Hii inaweza kuwafanya baadhi waone wivu na matokeo yake wanajenga chuki baina yao na wake za watoto wao. Hofu ni sababu nyingine. Baadhi ya mama wakwe wanahofu kuwa wake wa watoto wao wanaweza kubadilisha mawazo ya kijana wao wa kiume ili wasiendelee kuwahudumia kama zamani.

Hofu hii niliitolea mfano wiki iliyopita kwa wale wanaochukia waume zao wasihudumie tena familia zao. Eti mumuwe asitoe tena matumizi kwa wazazi au asisomeshe ndugu. Hivyo, hufanya juu chini kuhakikisha watoto wao hawawapi wake zao upendo halisi.

Tabia yako ni sababu nyingine. Kama nilivyotangulia kusema kuwa baadhi ya wake wana tabia zinazoweza kuwasukuma wakwe kuwachukia. Baadhi ya wake ni wachafu, wagomvi, wakorofi, wana wivu uliopitiliza na wengine siyo waaminifu katika ndoa zao.

Kama tabia yako ni mbaya, usitarajie kupendwa na mama mkwe wako! Hata kama mama mkwe wako hajasoma hupaswi kumdhihaki na kumdharau. Anapaswa kuheshimiwa na kama humpendi, mtoto wake naye hatokupenda.

Na kama siyo mwaminifu katika ndoa yako, unaweza kumwona kama ni “muuaji” maana atakuchukia sana kwa sababu anamlinda mtoto wake!

Sababu nyingine ni utasa. Kama ndoa haina watoto, mara nyingi ni rahisi sana kulaumiwa. Wanaweza kuanza kusema, “huyu mwanamke ni jangwa”. Hakuna mtu anaweza kumlaumu mwanamume. Utasa ni moja ya sababu inayowafanya wakwe wengi wawachukie wake wa wana wao.

Ujinga ni sababu nyingine. Wakwe wengi hawajatambua nafasi yao. Huamini nyumba ya watoto wao ni yao na kwamba wao ni wamiliki wa mali za watoto wao.

Hii mara nyingi husababisha migongano kati ya wakwe na wake wa wana wao, walio warithi halali wa mali za waume zao. Pia wazazi wa kale (wa kizamani) hawaelewi aina ya uhusiano unaofanya kazi siku hizi kati ya mke na mume!

Sababu nyingine ni upendo uliopitiliza juu ya watoto wao wa kiume. Mama wakwe wengine wapo karibu sana na watoto wao wa kiume. Hivyo, inakuwa ngumu kuvunja uhusiano wao pale watoto wao wanapoamua kuoa. Wakwe huanza kuona mke kama ni tishio!

Pia mama mkwe anaweza kukuchukia kwa sababu hakuwa chaguo lake kwa mtoto wake kuoa. Anaweza kukuchukia kwa sababu ya kabila lako kuwa tofauti na la kwao. Hata kama anakuchukiaje, unapaswa kuwa na hekima jinsi ya kuchukuliana naye.

Hii ya kabila tofauti katika ndoa zingine imesababisha mitikisiko mingi hata wengine kufikia hatua ya kuachana kabisa kwa talaka mahakamani. Ipo familia moja ndoa ilishavunjika kufuatia mikwara mingi.

Wazazi wa kijana hawakutaka mke amemzidi elimu kijana wao, wala awe na kazi nzuri. Ni familia iliyokuwa inataka mwanamke awe tu mama wa nyumbani kuhudumia watoto na wao wakwe.

Hata pale mke alipopambana kwa msaada wa wazazi wake na kupata digrii, bado hakuruhusiwa kufanya kazi. Mwanaume akawa anampiga mara kwa mara. Mke akakimbia, mume akadai talaka, ndoa ikavunjika.

***Wiki ijayo tutaangalia namna kumfanya mama mkwe akufurahie. Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Ana ndimi nyingi, sura nyingi na haaminiki

FURAHA haitibu majeraha. Lakini angalau inawanyima maadui zako mahali pa kuanzia, wakati upitapo kwenye majaribu. Si ndiyo eeh!

Na usikubali kutoa ahadi wakati una furaha. Majuto yake ni makubwa unapotaka au kutakiwa kutekeleza ahadi yako.

Licha ya kwamba wanasiasa vijana, wanatazamwa kama injini ya serikali au chama cha siasa katika taifa lolote lile duniani, bado wanakabiliwa na changamoto ya kuaminiwa.

Wengi wao wanakosa au kupoteza imani katika mamlaka za uteuzi, kutokana na kujisahau kwa kufanya uamuzi wa hivyo, au kushiriki mipango michafu.

Jambo la kupigiwa mfano hapa kwetu Tanzania vijana wengi wameaminiwa na kupewa nafasi nyeti za madaraka serikalini, lakini humo humo wamo waliokosa bahati ya kupita katika chungu cha ujenzi wa fikra.

Kukosekana huko kwa chungu maalum cha kuwapika vijana wanaochipukia katika siasa, ndicho kinachofanya leo hii tunakosa nguvu ya majadiliano ya kina yanayotawaliwa na nguvu ya hoja.

Mijadala yetu mingi huko kwenye mitandao ya kijamii, haikosi kushambuliana kwa maneno makali na haitoi taswira au mwanzo wa hoja nyingine kujijenga.

Kama vijana tunataka kuendelea kuaminiwa kushika nafasi nyeti serikalini au katika vyama vya siasa, tujitofautishe na akili za kushikiwa.

Leo yako, kesho yako ilenge kujielekeza kufanya mambo yanayoacha alama na si kutafuta ‘kiki’ ambazo mwisho wa siku hukumbukwi na wala hutoaminika tena.

Wako vijana, ukiwaona au kuwafuatilia nyendo zao, utabaini anachokitafuta ni zaidi ya uteuzi.

Mtu wa aina hii hafai kwenye manowari ya kivita, kwa sababu amekaa kimaslahi zaidi.

Kosa lingine la kimantiki, baadhi ya wanasiasa vijana hawajifunzi namna bora ya kujenga hoja, namna bora ya kuonyesha kutokubaliana, kukubaliana na namna ya kushinda.

Yuko mwanasiasa kijana, ukimwona au kumsikiliza ama kusoma maandiko yake kwenye mitandao ya kijamii, utagundua huyo ni zaidi ya msaka fursa.

Si dhambi kutafuta fursa, ila hoja ni kwamba utaitendeaje haki fursa hiyo utakapoitapata!

Wanasiasa wengi wa aina hii, dhamira yao, sura yao na mwonekano wao unaonyesha dhahiri shahiri ni watu wa kutaka wanachokitaka.

Ni kijana ambaye akishabaini kusema au kufanya lolote kutampa fursa, basi atatenda. Hataki kuona ukosoaji dhidi yake, hata kama kuna mantiki katika hoja fulani. Huko ni kujitengenezea tafsiri ya mtu mwenye ndimi nyingi, sura nyingi na ambaye haaminiki.

Ni jambo gumu lakini ni lazima tujitofautishe na wale walioharibu huko nyuma, taswira nzuri ya wanasiasa vijana, ambao waliaminiwa na kupewa nafasi nyeti za kuutumikia umma.

Labda kazi kubwa iko kwenye kujitofautisha na kujiweka kando na suala la mgongano wa maslahi.

Kufanikiwa kwako kutatokana na kuacha kudharau kufanyia kazi mlichokubaliana na walio juu yako au chini yako.

Achana na kufanya mashambulizi binafsi dhidi ya mwingine au wengine. Waza ndoto kubwa zaidi. Fikiri zaidi juu ya kutengeneza kitakachokuwa urithi toka kwako.

Kwanza, jenga uhalali wako, waaminishe unaowaongoza ama unaotaka kuwaongoza ili waelewe na kuamini kile unachokisema.

Jenga uhalali wako kwa kuwaondolea shaka ya mgongano wa maslahi na kile unachokisema.

Kwamba kwa nafasi uliyopewa uking’atuka au uteuzi wako kutenguliwa, utakuwa umeacha alama fulani ya kukumbukwa.

Mwalimu wangu katika somo la Falsafa, Mhadhiri Mwandamizi, pale Chuo Kikuu cha Iringa (UoI), aliniambia wakati fulani “ukitaka kumjua mwanasiasa anakipenda chama au hakipendi, mnyime madaraka anayoyataka, mnyang’anye haki yake ya kupata madaraka kwa njia ya kugombea halafu mkoseshe madaraka. Hapo sura nyingi alizonazo utaziona pasi na shaka’.

Aliongeza “...ukitaka kumjua zaidi, mpime imani ya itikadi aliyonayo, endesha mchakato unaonyima madaraka kwa makusudi. Utaona alivyo na ndimi nyingi’.

Inahitajika nguvu kuwasukuma wengine kuupenda ushawishi wako, kuukubali na kubadilika.


Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe Kanda ya Kaskazini.

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

***Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# Send-off









Shere-
he ya sendoff
ya Lucy Mwaitete
iliyofanyika Juni 18,
2023 katika ukumbi wa
JC Mbezi Beach Dar es
Salaam. Ndoa kati yake na
Moses Osani, inatarajiwa
kufungwa Julai 2, 2023
katika Kanisa la Wa-
sabato la New Life
jijini Nairobi
Kenya.





# MITINDO

Na Mary Geofrey





# FULANA INAPENDEZA

## kipindi cha kipupwe

KIPINDI cha kipupwe kinaendelea nchini kote, baridi la wastani linazidi kuleta usumbufu kiasi.

Hata hivyo, mwonekano wa mitindo unazidi kuleta furaha wakati huo huo unajikinga na hali ya baridi kila unapotaka kutoka.

Je! unavaa nini kutaka kukubiliana na hali ya baridi? Hilo ni jambo dogo, kwani baadhi ya fulana zinaweza kukusaidia na kukupatia mwonekano murua.

**Jinzi na fulana**

Unaweza kujaribu kitu cha kipekee kama kununua fulana mtandaoni inayopendwa na kuwa vazi lako muhimu.

Jinzi na fulana ni mwonekano mzuri katika msimu wa baridi

**Fulana kubwa**

Uvaaji wa fulana kubwa ingawa inaleta mwonekano mpana wa mitindo, bado inatikisa katika uzuri wa mtu wakati wa baridi.

Fulana kubwa, leggings na kanzu yoyote kwa mtindo wa michezo inapendeza zaidi.

Ikiwa wewe ni shabiki mkubwa wa fulana, unaweza kuchanganya na baadhi ya nguo zingine kama koti refu, au koti la kawaida na ukawa na mwonekano wa kupendeza.





## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# TUFAA, KITUNGUU SAUMU inavyong'arisha kucha







FANGASI ya kucha ni tatizo sugu linalowakumba idadi kubwa ya wanawake na hata wanaume.

Dalili zake ni kuvimba, maumivu ya hali ya juu, kucha kusinyaa au kuwasha.

Kama fangasi ya kucha haitachukuliwa tahadhari mara kwa mara huweza kusababisha kukatika kwa kucha na hata kuimaliza kucha na kutoka kabisa.

Habari nzuri ni kwamba fangasi ya kucha hutibika bila hata ya kutumia pesa kwa dawa za hospitali na ukabaki na urembo wako.

**Mafuta ya machungwa**

Njia nyingine ni kutumia mafuta ya machungwa ya aina zote za machungwa kutibu fungasi.

Kwa kudondoshea kitone cha mafuta hayo kila siku katika hapo penye fangasi, juu, chini na katikati ya kucha na iache kwa saa moja.

Pia unaweza ukachanganya hayo mafuta ya machungwa sawa na mafuta mengine yoyote kama mafuta ya mbegu za zabibu.

**Kitunguu saumu**

Kwa kutibu mara ya kwanza tumia mafuta ya kitunguu saumu changanya sawa na vinegar namaanisha kipimo cha vinegar na mafuta viwe sawa.

Kisha pakaa eneo la fangasi na pembeni yake kisha funga tumia bandeji. Ikiwa mafuta ya saumu hayapatikani, tengeneza mwenyewe kwa kusaga, chukua vitunguu saumu viwili kisha changanya na vijiko viwili vya kula vya olive oil, kisha iache kwa saa 24.

Hata kula kitunguu saumu kimoja kila siku nayo ni dawa ya fangasi pia.

**Juisi ya siki ya tufaa**

Juisi ya siki ya tufaa (apple) ina acid ya asili na huweza kulinda na fangasi ya kucha kuendelea.

Chukua juisi ya siki ya apple changanya sawa kwa sawa na maji kwa kipimo chochote utakachotumia.

Kisha utaitumia kwa kuloweshea sehemu ya fangasi kila siku kwa muda wa nusu saa.

Kama utafanya hivi kwa muda wa wiki kadhaa utao- na mabadiliko kwa muda mfupi.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Vitumbua vya nazi

LEO nimewaandalia jinsi ya kupika vitumbua. Hiki ni kitafunwa kinachopendelewa kwa chai.

Vitumbua vinatokana na unga wa mchele na kinapendeza zaidi kuliwa nyakati za asubuhi na jioni.

**Mahitaji**

Mchele kilo moja, nazi kubwa mbili, hiliki kiasi, sukari robo kilo, hamira kiasi kijiko kimoja na nusu ( itategemea aina ya hamira), mafuta nusu lita na mayai matatu (ukipenda).

**Jinsi ya kupika**

Loweka mchele uliokwisha uchambua vizuri na kuupeta na utandaze sehemu safi ukauke, kisha usage upate unga mlaini.

Kuna nazi uchuje tui zito, saga hiliki, changanya na sukari na changanya ule unga wa mchele, sukari, hiliki, tui la nazi na hamira.

Uvuruge uwe mwepesi kiasi cha kuchoteka kwa upawa. Acha uumuke kwa dakika 25 hadi 30 kutegemea na ubora wa hamira.

Weka kikaango cha kukaangia vitumbua jikoni, anza kukaanga vitumbua vyako kwa kuweka mafuta kwanza yapate moto, kisha unachota kwa upawa unga na kuweka kwenye vijungu vya kikaangio.

Unaacha vichemke upande mmoja, kisha unageuza upande wa pili, vikishaiva vitoe weka kwenye chujio ili mafuta yajichuje. Endelea kukaanga vilivyobakia mpaka unga uishe.

Vitumbua hivi vinaweza kuliwa na chai, maziwa, uji na hata juisi ukipenda, ukivipata bado vimoto huwa safi sana.





MAISHA NI NYUMBA

## Tambua tofauti ya taa ndani ya nyumba

**Na Restuta James**

UCHAGUZI wa taa za ndani na hata nje, ni moja ya eneo linalowapa watu wengi changamoto kutokana na ukweli kwamba zinachukuliwa kama kitu cha ziada.

Mtaalamu wa masuala ya umeme, Deus Willomi, anasema uchaguzi wa taa ni eneo ambalo linapaswa kupewa uzito wa pekee kwa kuwa litaamua matumizi ya umeme kwa muda mrefu.

Anasema imekuwa kawaida kwa watu kununua taa kwa kuzingatia urahisi wa bei na mwonekano, bila kuangalia matumizi yake ya umeme.

"Ninachoweza kushauri ni kwamba unaponunua taa zingatia zile za teknolojia ya LED ambayo inapunguza sana matumizi ya umeme," anasema.

Deus anasema zipo taa nzuri za sehemu ya kulia chakula, sebule, vyumbani, ukutani na bustani, ambazo zinatumia teknolojia hiyo.

Anashauri kwamba 'warm white' ndio rangi mujarabu kwa chumbani wakati 'cool white' ni kwa ajili ya sehemu ya chakula na day light ni mahsusi kwa ajili ya jikoni.

Kwa upande wa nje, Deus anasema warm white ni sehemu yake japokuwa unaweza kuchanganya (RGB-red, green and blue), kulingana na mtu anavyopenda.

Jambo la msingi analolisisitiza mtaalamu huyo ni kupunguza matumizi ya umeme yasiyo ya lazima kwa kuchagua bidhaa za teknolojia ya LED.



**Na Elizabeth Zaya**




# Zilivyo kero za madalali wa nyumba za kupanga

NI kawaida watu wengi wanapokuwa wanatafuta nyumba kwa ajili ya kupanga kwa matumizi ya makazi, biashara au kununua hutumia madalali ambao ni wabobezi katika eneo hilo.

Pamoja na kupendelea kuwatumia madalali hao, lakini wengi wao wamekuwa wawalalamikia kwamba ni kero.

Na leo tunaangazia sauti za watu hao ambao wanalalamikia kero wanazokutana nazo kwa madalali hao.

Wa kwanza anasema "Kiukweli ninakerwa sana na madalali wa nyumba za kupanga. Kwanza ninataka kujua hii sheria yao ya kuwapa kodi ya mwezi mmoja wanapokutafutia nyumba, imepitishwa na nani, na je, wanalipa kodi kwa serikali tunapowapa hiyo kodi ya mwezi mmoja?

"Na hii sheria ya kupelekwa kwenda kuona nyumba au chumba kwa Sh. 5,000 au 10,000 nani kaipitisha? Nimeandika hivi kwa sababu usumbufu tunaoupata wakati wa kutafuta nyumba ni mkubwa mno. Madalali wengine ndio wamekuwa kama wenye nyumba, hadi bei za nyumba wanabadilisha.

"Wanawashauri wenye nyumba kubadilisha au kuongeza kodi ili wapate fedha kubwa. Ikumbukwe kwamba dalali ni daraja la watu wawili, mwenye nyumba na mpangaji, lakini inakuwaje jukumu la kulipa hiyo fedha ya mwezi mmoja lisiwe la wote wawili, kwanini aachiwe mpangaji peke yake?

"Ama walipe wenye nyumba tu na sio wapangaji maana wao wanahangaika sehemu ya kujihifadhi. Maskini ya Mungu unakuta alikotoka amefukuzwa kwa kushindwa kulipa kodi ila cha ajabu zaidi anakokwenda anatakiwa alipe kodi ya miezi mitatu hadi sita na kodi ya dalali juu pamoja na Sh. 5000 au 10,000 kila nyumba anayopelekwa kuiona."


Mwingine anataja baadhi ya kero zinazomtesa kutoka kwa madalali ni kile anachokiita tabia yao ya kutokupenda kusema ukweli.

"Lipo tatizo la uongo kwa madalali wengi, unamweleza kwamba ninataka nyumba ya aina fulani, anakuambia njoo ninayo, ukimwomba akutumie picha, anakuambia 'niko mbali kidogo na sijapiga picha'. Ukija utaiona mwenyewe lengo tu apate hiyo Sh. 10,000 yake. Utaambiwa nyumba iko karibu na barabara. Sasa ukienda utajuta kumfahamu, kiukweli inakera sana.

"Ninadhani ifike wakati serikali iingilie kati, upangishaji wa nyumba na hili la madalali, nyumba za kupangishwa ziwekwe kwenye mfumo rasmi ili kodi zisiwe za kukomoana.

"Kiukweli ukiongelea ugumu wa maisha suala la kodi za nyumba lazima ulitaje na wenye nyumba nao wanavimba vichwa mno."

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
HA HA HAAA! BOSI NIPO KIJIJINI NDIO TUPO MAKABURINI TUNAZIKA NTAREJEA KESHO
DUH! MSHUA UTAFIKA LAKINI NYANG'ANYANG'A
JUKWAANI
NGUMI ZA DEMU WA KIZARAMO HUWA HAZICHOKAGI HIVYO WEWE TUSIDANGANYANE 'NI KANDA MAALUM!"
KILANGA KOMO! NILIKWAMBIA HARUSI YA MJEDA HATUWEZI KUZAMIA UKABISHA!
TUNGEPATA WAPI CHA KUSIMULIA VIBAO NA MITAMA YA UKUBWANI
SHOSTI MIMI SIO WA KUPWIANGA KUTAFUTA MADANGA EMBU NIPE HESHIMA YANGU NIJITULIZE NIOLEWE
UOLEWE NA NANI ZAIDI YA KUSUBIRI PALAPANDA!
SI MMESIKIA KUINGIA BURE KUTOKA BURE NO, MALIPO
MCHECHETO NI KITU KIBAYA NDUGUYO AKIWA NDANI UNAKWENDA NA HELA ' UMETUMWA?!
ENDELEENI NA SHOBO ZENU NAONA MNAHAMU NA LUPANGO MKALE UPEPO
HERI MIMI NILIYEJIKALIA KIMYA KAMA SIPO HUMU!
NANI ALISEMAGA TULIPE?
HUO UTAMADUNI MMEJIJENGEA KWA KUOGOPA 'MANJAGU' ALAFU LEO MNAJISHAUA!
AHERI YA SISI WALALA HOI KULIKO WAO WA USHUANI TABU TUPU!
UNAACHA ILE BENZI INAOTA KUTU IMEKAA HUTEMBELEI SI BORA TUMPE HAUSI GELO?
TENA NYAMAZA USIYEISHIWA SAFARI ZA SHUGHULINI
SIENDI POPOTE HATA ILE HARIA NISHAICHOKA MPE ZOTE
WE MWANAMKE UTANIKAUSHA DAMU NIACHE NIKAKAE NA MWANDANI WANGU NIJITAFAKULI...
NENDA 'DANGA' ZEMBE
RUDIA NAHISI SIJAKUSIKIA UMENAMBIAJE!
MUME WANGU KARUDI NAOMBA UMRUDIE MKEO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...TUTAGAWANA KILA KITU, LAKINI SIO UMASIKINI...

# UASI WAITISHIA RUSSIA, NCHI YATAHADHARISHWA

## - Wagner wateka sehemu ya nchi
## - Putin aapa kuwashikisha adabu



Rais wa Russia, Vladmir Putin



Kiongozi wa Kundi la Mamluki la Wagner, Yevgeny Prigozhin.

**MOSCOW,** RUSSIA

HALI imekuwa tete nchini Russia, baada ya kundi la mamluki wa kijeshi Wagner kuasi na kuteka mji ulio kusini mwa nchi hiyo Rostov-on-Don hapo jana.

Rais wa Russia, Vladimir Putin, akitoa hutuba kali alionya kuwa adhabu kali itachukuliwa dhidi ya wale wanaogawanya jamii ya nchi hiyo.

Aliongeza kwamba kutaongezwa vikosi vya kukabiliana na ugaidi katika mji mkuu wa Moscow na mikoa mingine kadhaa.

Katika hotuba yake kwa taifa kupitia Televisheni, Putin alisema mustakabali wa Russia uko hatarini, na kuelezea vitendo vya waasi uliotokea sawa na usaliti.

Bila kumtaja kiongozi wa kundi la Wagner, Yevgeny Prigozhin, Rais Putin alisema matamanio makubwa ya baadhi ya watu yamesababisha uhaini mkubwa.

Kiongozi huyo alisema baadhi ya Warussia wamedanganywa na kuingizwa katika tukio la uhalifu bila kulitaja kundi la wapiganaji wa Wagner.

WAGNER WAJIBU

Ujumbe wa sauti uliochapishwa haraka kwenye mtandao wa kijamii wa Telegram wa kundi la Wagner mara baada ya hotuba hiyo na kusema Rais Putin alikosea kutaja kitendo hicho kuwa usaliti.

Ujumbe huo unaonekana jibu la moja kwa moja na la dharau kutoka kwa Yevgeny Prigozhin, mkuu wa kikundi cha mamluki.

Sauti ya kiume inayofanana na ya Prigozhin ilisikika ikisema "Kuhusu uhaini wa nchi, rais alikosea sana. Sisi ni wazalendo wa nchi yetu, tumekuwa tukipigana na tunapigana hata sasa,"

Sauti hiyo iliongeza "Na hakuna mtu atafanya kama anavyotaka rais, FSB (huduma ya usalama ya Russia) au mtu mwingine yeyote, tukubali makosa yetu,".

Ikasisitiza "Kwa sababu hatutaki nchi yetu iendelee kuishi katika ufisadi, uwongo na urasimu."

Katika ujumbe uliotumwa kwenye mtandao wa Telegram Jumamosi asubuhi, Yevgeny Prigozhin alisema kwamba wanachama wote wa kundi lake la mamluki la Wagner walikuwa tayari kufa katika hatua yake dhidi ya jeshi la Russia.

"Sote tuko tayari kufa. Wote 25,000, na wengine 25,000," alisema katika ujumbe wa sauti, akiongeza hatua hiyo inachukuliwa kwa niaba ya watu wa Russia.

### TAHADHARI YAONGEZWA

Meya wa jiji la Moscow ametangaza hatua za kupambana na ugaidi zinachukuliwa ili kuimarisha usalama katika mji mkuu.

Katika chapisho kwenye Telegram, Sergey Sobyanin aliandika, "Kuhusiana na yale yanayojiri, hatua za kupambana na ugaidi zinachukuliwa huko Moscow zinazolenga kuimarisha hatua za usalama.

"Udhibiti wa ziada wa barabara umeanzishwa.Hali hii inaweza kuathiri shughuli za umma. Tafadhali zingatia hatua zilizochukuliwa kwa makini." Aliongeza kusema.

### KUTUNISHIANA MISULI

Mamlaka nchini Russia na mkuu wa kundi la mamluki la Wagner, Yevgeny Prigozhin, zinaonyesha haziko tayari kulegeza kamba katika mzozo huo ambao sasa unaelekea kutishia nchi hiyo.

Mara kwa mara Prigozhin, alimwelekezea lawama Waziri wa Ulinzi wa Urusi, Sergei Shoigu, kuwa vikosi vya jeshi la nchi hiyo vilishindwa kwenye uwanja wa vita huko Ukraine.

"Vita vilihitajika ili Shoigu aweze kuwa mkuu wa jeshi, ili aweze kuwa shujaa wa pili,vita havikuwa vya kudhibiti shughuli za kijeshi au kuiondoa Ukraine. Ilihitajika kwa malengo ya ziada," alisema Prigozhin.

Pia alilaumu vita dhidi ya watu mashuhuri wa Russia, akilaani ukoo ambao kiuhalisia unatawala Russia mpaka sasa.

Aidha kauli yenye utata zaidi ni ile ya madai ya Prizoghin kwamba kambi ya Wagner nchini Ukraine ilishambuliwa na jeshi la Russia mapema wiki hii.

Hata hivyo, Wizara ya Ulinzi ilikanusha madai hayo.

Wachambuzi wa Kremlin pia wanaashiria chuki ya kibinafsi ya muda mrefu kati ya Prigozhin na Shoigu, ambao majenerali wao wanamwona mkuu wa Wagner kama mgeni mwenye uchu wa madaraka. Lakini mpaka sasa, Prigozhin aliyepewa jina la utani "mpishi wa Putin" kwa mikataba ya upishi ya zamani kutoka Kremlin haijaelekeza changamoto ya moja kwa moja kwa utawala wa Putin.

### MJI WA ROSTOV

Katika mji wa Rostov-on-Don, imeshuhudiwa magari ya kijeshi ya kivita yakisambaa mitaani.

Mji huo uko zaidi ya kilomita 1,100 sawa na maili 680 kusini mwa mji mkuu wa Moscow.

Awali, Prigozhin, vikosi vyake sasa vinaudhibiti mji huo.

Wakazi wa eneo la Rostov linalopakana na Ukraine wametakiwa kusalia majumbani kwa sababu vikosi vya usalama vinafanya kazi katika eneo hilo.

Mkuu wa kundi la mamluki la Wagner Yevgeny Prigozhin ameapa kuondoa uongozi wa jeshi la Urusi na kusema kuwa vikosi vyake vimevuka hadi Urusi kutoka Ukraine.



Wapiganaji wa Kundi la Mamluki la Wagner wakiwa wamezingira, Makao Makuu ya Jeshi katika jiji la Rostov-on-Don. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

MAKALA

# UZALENDO SI HAKI YA VIONGOZI PEKEE



Na Magabilo Masambu

**Katika mjadala wa bandari yamezungumzwa mengi lakini ukisikiliza kwa makini wazungumzaji wote wamegawanyika kulingana na nia inayowasukuma kuzungumza. Nimpongeze Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa kauli yake ambayo ninaamini ni kauli ya serikali I hawatodharau maoni ya wananchi, iwe wamezungumza kwa nia njema au mbaya, maoni ni maoni.**

NENO uzalendo limekuwa likipewa tafsiri nyingi. Wapo wanaoamini mzalendo ni mtu masikini asiyependa kujitajirisha, ndiyo maana hata nyakati za uchaguzi viongozi wengi huwaambia wananchi wawachague eti kwa sababu wao ni watoto wa masikini na kwamba shida wanazijua.

Baadhi ya viongozi wetu wamekuwa na imani kwamba wao pekee ndiyo wanaotakiwa kuzungumzia masuala ya nchi hii na hasa yanayohusu maslahi ya taifa na kwamba ni wazalendo kwa sababu wanayo mamlaka mikononi. Jambo wanalotakiwa kufahamu ni kwamba, uzalendo siyo haki ya viongozi pekee, bali kila mtu ndani ya nchi anapaswa kuwa mzalendo na taifa hili.

Inapofika hatua kiongozi aliyekabidhiwa dhamana ya kuongoza na wananchi, akaona anayo haki zaidi kuliko wananchi wenyewe, maana yake anataka kuongoza mbadala wa wananchi na siyo kwa niaba ya wananchi. Tabia ya kuona una haki zaidi yako ni tabia ya unanifsi aliyoisema Mwalimu Julius Nyerere katika kitabu chake cha 'Tujisahihishe', ni tabia ya kila mtu tofauti yake ni kiwango cha unabifsi.

Mamlaka hayamfanyi mtu awe mzalendo zaidi, akiwa si mzalendo hawezi kujifunza uzalendo akiwa na madaraka, bali kuna hatari ya kutumia mamlaka yake kujinufaisha huku akiwataka wengine wakae kimya, hawana haki ya kushiriki katika ujenzi wa taifa lao kwa sababu hawana madaraka. Jambo la msingi hapa ni muhimu kufahamu chakula kinaiva jikoni si kwa sababu ya moto mkali unaowaka, bali miti au mkaa uliotumika kuwasha moto wenyewe.

Katika mjadala wa bandari yamezungumzwa mengi lakini ukisikiliza kwa makini wazungumzaji wote wamegawanyika kulingana na nia inayowasukuma kuzungumza. Nimpongeze Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa kauli yake ambayo ninaamini ni kauli ya serikali I hawatodharau maoni ya wananchi, iwe wamezungumza kwa nia njema au mbaya, maoni ni maoni.

Kauli ya Waziri Mkuu inadhihirisha serikali ilikuwa na nia njema kuweka wazi makubaliano hayo kati yake na DP World. Kama isingelikuwa na nia njema ya kutaka kupata maoni ya wananchi, makubaliano hayo yangelifanyika sirini baadaye tungeona matokeo tu.

Kwa hiyo, ni muhimu pia watanzania wenzangu kuiona nia hiyo njema ya serikali na kutumia sasa nafasi hiyo kukosoa na kutoa mapendekezo ya namna uwekezaji huo unavyoweza kulinufaisha taifa, badala ya kuliangamiza kama inavyosemwa sasa.

Katika mazingira ya ulimwengu wa leo, ukweli wa taarifa ni ngumu kumilikiwa na kundi moja pekee, bali kwa nyakati tofauti makundi tofauti yanapata taarifa tofauti, kutoka sehemu tofauti duniani. Kila linalozungumzwa kuhusiana na kampuni hiyo, siyo la kupuuza hata kidogo, liwe limezungumzwa na mlevi, ni la kufanyia kazi badala ya kulibeza.

Ni kweli kwamba serikali inafahamu zaidi kuhusu tatizo lililopo badarini, lakini ukisikiliza maoni ya watanzania utagundua kwamba matatizo ya kikodi, urasimu, rushwa na watu kutowajibika yamekuwapo jkwa muda mrefu bandarini.

Sasa sjui kama matatizo hayo nayo yanahitaji mwekezaji, yaani kwa maana nyingine tukishindwa kuwachukulia hatua tunatafuta mwekezeji ili wao wasiwapo na wahamie sehemu nyingine? Hili nalo linaweza kuwa tatizo. Kubwa zaidi kuliko la uwekezaji lenyewe. Kuna mizigo ambayo haihitaji kupakuliwa kwenye meli lakini utokaji wake bandarini ni tatizo kubwa, kodi za kubambikiza nazo zinatajwa.

Binafsi ninaona jambo hili tunakwenda vizuri, tuondowe hisia za kushutumiana ambazo ziko nje ya jambo lenyewe, turekebishe penye upungufu, tuondoe mtazamo wa kwamba wanaojadili wanakusudia kutukwamisha, mkataba ulitolewa wazi ili watu wajadili na hivyo siyo sahihi kuwapangia cha kujadili, bali ni kusikiliza kama kuna haja ya kubadili au ubaki hivyo hivyo, kitu ambacho si lengo. Tuaminiane tupendane. Sisi ni Tanzania.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Pili Mswahili, mrembo wa Kibongo aliyemchanganya mwanamuziki Kenya*



Na Adam Fungamwango

**Wakongomani ndiyo kabisa, walikuwa na bendi nyingi zikiongozwa na Orchestra Les Mangelepa, Super Mazembe, Bana Ngenge, Boma Liwanza na nyingine nyingi. Moja kati ya santuli kutoka Kenya zilizofanya vema sana ilikuwa ya wimbo uliofyatuliwa mwaka 1986, 'Pili Mswahili.'**

MWAKA 1986, ulikuwa na nyimbo nyingi zilizoingia nchini Tanzania kutokea Kenya kwa njia ya santuli. Santuli hizo ziliingizwa nchini na kuuzwa kama njugu maeneo ya katikati ya Dar es Salaam, hasa Kariakoo, mitaa ya Uhuru na Msimbazi.

Wakati Tanzania kukiwa na zaidi ya bendi 100, zilizokuwa zikipiga muziki wa dansi toka mikoa yote nchini, Kenya nayo ilikuwa haishikiki.

Ukiachia mbali bendi za Wakenya wenyewe, kulikuwa na bendi za Watanzania ambao walikuwa wakitoka nchini kwenda huko kusaka malisho bora.

Bendi za Simba Wanyika, Les Wanyika, Wanyika Stars, Nairobi Matata, zote hizi zilikuwa na wanamuziki wa Kibongo.

Wakongomani ndiyo kabisa, walikuwa na bendi nyingi zikiongozwa na Orchestra Les Mangelepa, Super Mazembe, Bana Ngenge, Boma Liwanza na nyingine nyingi.

Moja kati ya santuli kutoka Kenya zilizofanya vema sana ilikuwa ya wimbo uliofyatuliwa mwaka 1986, 'Pili Mswahili.'

Wabongo wengi waliupenda na kuucheza kwenye hafla mbalimbali za kiserikali na kijamii, lakini si wengi waliokuwa wanafahamu ulitungwa na nani, bendi gani na kwa sababu gani.

Wimbo huo ulitungwa na mwanamuziki Moreno Batamba raia wa Kidemokrasi ya Congo.

Ni mmoja wa wanamuziki wachache wa Kikongomani ambao nyimbo zao nyingi amezitunga na kuziimba kwa lugha ya kiswahili.

Moreno, aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Orchestra Moja One alitunga nyimbo mbalimbali kwa lugha hiyo kama vile 'Dunia Duara', 'Urembo si Hoja', 'Mwanamke Hatosheki', 'Angela', 'Danger Girl', 'Mapenzi ya Shida', na nyingine nyingi.

Alikuwa na asilimia chache sana za nyimbo ya Kikongomani, lakini yeye alijikita kwenye kiswahili zaidi. Mwanamuziki huyo alikifahamu kiswahili kwa sababu aliwahi kuishi nchini Tanzania mwaka 1978 hadi 1980 akitokea nchini kwao Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kujiunga na bendi ya Orchestra Safari Sound (OSS). Si wengi wanaoelewa hili kuwa Moreno aliwahi kuishi jijini Dar es Salaam.

Aliondoka nchini akiwa si maarufu, na kwenda nchini Kenya kuangalia maisha mengine, na huko ndiko nyota ilipomuwakia, kwani milango ikafunguka na kuwa mmoja wa wanamuziki maarufu mno, si nchini Kenya tu, bali Afrika Mashariki na kati yote.

Pili Mswahili ni nani? Huyu ni mwanadada mrembo wa Kitanzania aliyewahi kuwania Umiss Tanzania miaka ya nyuma, Pili Mikendo.

Mwanadada huyu baadaye alikwenda kuishi nchini Kenya, ndipo alipokutana na mwanamuziki huyo na kuwa wapenzi.

Moreno alipenda kumtania mpenzi wake kwa jina la Pili Mswahili, kwa sababu ni Mtanzania na imekuwa ni sifa kubwa ya Wabongo sehemu mbalimbali duniani wanapokwenda kuwa ni wajanja na wanaongea sana.

Mwanamuziki huyo alifariki dunia mwaka 1993 Nairobi nchini Kenya akiwa kijana tu wa miaka 38.

**Leo tunayaangalia mashairi ya wimbo huo 'Pili Mswahili' ambao Moreno alimtungia mwanadada huyo.**

*"Mimi sielewi, nifanye nini, ooo mama, Pili yeye eeee, mapenzi ya safari, yamenichoka aa, leo mimi kesho yule sitoweza.*

*Pili yeye eee, Pili mtoto wa Tanzania aaha, Pili we mswahili iii, ujanja mwiiingi eee.*

*Usiku na mchana ninakutafuta, ninauliza uko wapi, Magomeni eee, Mapipa eee, Mapipa eee, Chang'ombe.*

*Unieleze mama yoyo yoyo ooo, Pili eee, mbona mimi sikuelewi hihi, Pili sema ukweli wako, amua weewee*

*Usiku na mchana mimi sitoweza, nakutafuta sikuoni, jamani eee, popote natafuta eee, ma...*

*Unieleze mama yoyo yoyo ooo, Pili eee, mbona mimi sikuelewi hihi, Pili sema ukweli wako, amua weewee*

*Pili eee, nasema mpenzi unielewe, unieleze nipate kujua.*

*Unieleze nipate kujua, ukweli useme daima mama, mapenzi gani hayo imekuwa kampuni ee, kampuni oo ya nini eee, Pili yoyo, Mikendo eee*

*Pili eee, nasema mpenzi unielewe, unieleze nipate kujua.*

*Rohoni nafsi unapenda wangapi ooo, rohoni nafsi sababu ndiyo pesa, mapenzi gani shirika ni ya nini? Waleta aibu kwa wazai wako ee, umenitoa hamu ya kukupenda.*

*Pili eee, nasema mpenzi unielewe, unieleze nipate kujua.*

*Unielewe, ooo mama, Pili mtoto ya Tanzania, Pili mtoto ya Dar es Salaam, Pili wewe mswahili, bibi mswahili eee*

*Pili eee, nasema mpenzi unielewe, unieleze nipate kujua."*

Hii inadhihirisha kuwa wanamuziki wengi wa zamani wa dansi walikuwa wakitunga nyimbo za matukio ya ukweli, ambao yametokea, au majina ya watu ambao ni kweli wapo hai na si ya kufikirika.

Na hii ndiyo inasemekana kuwa sababu ya nyimbo nyingi za zamani kuendelea kuishi na kupendwa hata kama zimeishi zaidi ya miaka 60 iliyopita.

**Tume meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




LEO amemuona laivu mwanamke aliyekuwa akimtolea maneno yale yaliyomchoma akachomeka. Huyo ndiye aliyedhania kuwa ni mke mwenzake.

"Mhh! Mbona hafanani? Mwanamke ana maneno mabovu hivi." Akajiambia mwenyewe. Lakini hapo hapo akajikumbusha kuwa ilikuwa ni zamu yake na yeye kuongea. Tena yeye ndiye anasubiriwa kuwa mwamuzi wa kisa kizima na mbinu iliyofanywa na Belo pamoja na Massawe kuwakutanisha hapo kwenye sherehe.

Ni kama mtu aliyekuwa hajajiandaa aseme nini. Alionekana kama mtu mwenye furaha, mshangao, huzuni, kwa wakati mmoja. Kila alichokisikia hapo kilikuwa ni 'sapraizi' kwake. Kuna wakati alitamani kulia, au kucheka. Akabakia kutofanya vyote viwili.

"Mabibi na mabwana." Husna alianza kwa sauti iliyoonekana ya chini sana. "Kusema kweli haya yote yanayotokea sasa yananishangaza. Hivi najiuliza ni ndoto au kweli? Ni kweli kabisa mimi nilipigiwa simu ya mtu niliyemjua akajitambulisha hawara wa mume wangu, akaongea maneno ambayo si vema kuyarudia. Binafsi sidhani kama yeyote angejua vinginevyo. Kwa hasira nikakurupuka kwenda ukweni, kwa wifi na shemeji yangu Belo. Nilichokwenda kubwata huko nakijua mwenyewe, maana siku hiyo nilivurugwa haswa. Aliporudi mume wangu nilimpakia ya kumpakia, nikaondoka kwenda kwetu na mpaka siku hiyo sijarejea tena. Naendelea kudai talaka yangu. Ila sijapewa hadi leo mwenzangu," vicheko vilifuatia baada ya neno hilo la mwisho.

"Nakumbuka, baada ya maneno ya mwisho niliyochambwa, nilizima simu, nikaifungia kabatini na hadi leo imo humo sikuichukua tena. Aliporudi nilimsusia nikamwambia sitoichukua tena simu kwa sababu alikuwa ameninunulia yeye na laini yake nikamuachia. Nikamwambia nikiendelea kuwa na simu yako hawara yako ataendelea kunisumbua, nikasajili laini yangu, nikanunua simu nyingine kwa sababu tayari nilikuwa nimepata pesa ya upatu, nikajiondokea zangu kwa mama yangu mdogo. Huyu hapa nimekuja naye, mama hebu simama wakuone."

Tabia alisimama na kupungia watu waliohudhuria, wakampigia makofi. Akaketi kwenye siti yake.

"Huyu ndiye mama yangu aliyenilea na hata mume wangu alinikuta kwake, akanioa nyumbani kwake. Nilikaa kwetu, akaja mume wangu kuniomba msamaha lakini mimi sikukubaliana naye. Akili yangu ilikuwa inahitaji talaka tu, siwezi kudhalilishwa vile.

> **"Huyu ndiye mama yangu aliyenilea na hata mume wangu alinikuta kwake, akanioa nyumbani kwake. Nilikaa kwetu, akaja mume wangu kuniomba msamaha lakini mimi sikukubaliana naye. Akili yangu ilikuwa inahitaji talaka tu, siwezi kudhalilishwa vile.**

Kweli kazi kubwa imefanyika, vinginevyo mimi nisingeamini chochote. Angekuja shemeji yangu tu na Massawe, sijui na nani aniambie kuwa simu imebadilishwa kwa fundi, kamwe nisiangeamini, ningejua kuna mchezo tu umechezwa hapa na kuna watu wamelipwa kwa sababu hii.

Haiwezekani mtu anakupigia simu anakwambia alitaka aolewe yeye mimi nimeingilia kati na ananitisha sitokaa kwenye ndoa kwa amani, nikiangalia ni kweli ndoa yangu ina miezi mitatu tu. Halafu anakwambia mumeo ninaye mimi hapa, na kweli mume wangu hayupo, kaniacha kaniambia anakwenda Zanzibar, kweli uache kuamini? Halafu kirahisi tu mtu au watu wawili watatu wanakuja nyumbani au wanakwita kwa pamoja kukuambia yalitokea kwa sababu simu zilibadilishwa, kusema kweli nisingeamini milele.

Lakini kwa staili hii aliyoitumia shemeji Belo na Massawe kushawishi na kuialika watu kwenye 'bethdei' wakiwemo wahusika wote wa tukio hili na wamelieleza kwa ufasaha, basi nimeamini." Mayowe ya furaha aliingia Dan pamoja na kijana mmoja. Kuna wakati alitoka nje.

Yule kijana akapitiliza moja kwa moja mpaka kwa Husna, akamkabidhi simu.

"Samahani wapendwa, hapa nimeletewa simu. Wakati tunaongea hapa, imekwenda kuchukuliwa nyumbani na mume wangu nilipoifungia kwenye kabati. Siku ile nilidhani ya kwangu, kwa sababu niliiangalia kwa haraka haraka na kuchanganya na ile hasira ndiyo kabisa. Hapa naiangalia, ni kweli siyo ya kwangu. Na laini pia si ya kwangu. Sasa naomba kwa heshima ya mzee Massawe na shemeji Belo nimwite dada Pendo pale aje hapa, nikabidhi ya kwake na yeye ya kwangu." Vilifautia vigelegele na nderemo.

Pendo alisimama na kwa sababu hakuwa amekaa mbali sana, alisogea hatua kama sita kwenda pembeni, akakutana na Husna. Wakakumbatiana. wahudhuriaji wakazidi kushangilia.

"Pole mwenzangu kwa yaliyokukuta." Pendo alimnong'oneza.

"Ahsante sana."

"Ndiyo ukubwa mwenzangu, ndoa zina changamoto, si unaona, hayo yaliyokukuta ndiyo yamenikuta mimi. Hiyo simu uliyopigiwa ilikuwa ya kwangu. Kilichokukuta ndiyo hicho hicho kilichonikuta, na mimi pia nilikuwa nimeonelewa muda si mrefu na mume wangu pia alikuwa hayupo, ndiyo maana kila kilichozungumzwa kilikuwa kinakugusa moja kwa moja."

"Mwenzangu, mbona makubwa." Husna akajibu huku kila mmoja akimpa mwenzake simu yake. Simu zilizobadilishwa kwa fundi simu na kuzua tafrani kwenye ndoa ya Dan.

Belo alinyanyuka akionekana ana jambo.

"Naomba pia, Zawadi uende kwa wenzako pale, nawe upate picha ya pamoja na wenzako."

Zawadi naye alinyanyuka na kuwafuata Husna na Pendo.

"Husna, huyu ndiye aliyekuwa mgomvi wangu, na ndiye aliyekupigia wewe akidhani ni mimi. Mimi nimemsamehe kwa yote juu ya mume wangu na sasa hivi tupo pamoja, ni shoga yangu hatari, naomba na wewe umsamehe."

"Pendo mimi nimemsamehe kwa sababu kumbe alikuwa anadhani anaongea na mtu mwingine."

"Nisameheni wote wawili, waswahili wanasema wagombanao ndiyo wapatanao." Zawadi aliomba msamaha huku wakiwakumbatia wote wawili. Wapiga picha za mnato na video walikuwa wanachukua kumbukumbu. Wenye simu janja nao hawakuwa nyuma. Kila mtu alikuwa anarekodi anavyojua yeye.

"Na kama mmenisamehe shoga zangu, mwezi ujao nafunga ndoa nawakaribisha wote wawili mje, yaani mkija nitafurahi mimi, na nitaona kweli mmenisamehe ili tujenge urafiki ndugu." Zawadi aliomba.

"We lete sare bibi, mimi ndiyo shughuli zangu hizo, nitazoa shoga zangu kutoka Mabibo na Mburahati, hutoamini." Wote waliangua vicheko kwa furaha kama vile wanafahamiana muda mrefu kiasi cha kuwashangaza wote mle ndani.

"Siku hiyo nitacheza kama mama yake mwali." Pendo alidakia na kuwafanya wafurahi zaidi.

ITAENDELEA JUMAPILI

# Young Thug atoa Albam akiwa kizuizini

RAPA wa Marekani, Young Thug ambaye anapambania uhuru wake baada ya kuwekwa kizuizini wakati akikabiliwa na kesi YSL RICO, ametambulisha albamu yake mpya ambayo ameita kama 'Business Is Business'.

Albamu hiyo yenye nyimbo 15 ni ya kwanza ya pekee kwa Thugger tangu alipotoa Punk ya 2021.

Ndani ya Albam hiyo kuna baadhi ya wanamuziki mastaa walioshirikishwa kama vile Drake, 21 Savage, Future, Lil Uzi Vert, Travis Scott na wengine.

Kinachoonekana kukosekana kwenye orodha ya nyimbo ni rapa Gunna, ambaye bila shaka itasababisha uvumi zaidi kuhusu hali ya sasa ya uhusiano wa wanamuziki hao maarufu.





# SAMPA MUSIC AFRICA LEBO YENYE MAPINDUZI

WAWEKEZAJI wengi kwenye tasnia ya muziki huwa wanalenga kupata faida zaidi kutoka kwa wasanii wanaowapa dili za usimamizi chini ya lebo wanazozimiliki.

Lebo nyingi zinajikita kuibua na kuwasimamia wasanii wanaofanya aina moja ya muziki inayofanya vizuri sokoni na kuachana na mamilioni ya vijana wenye vipaji vikubwa kwa sababu hawafanyi muziki usio na biashara kubwa.

Tazama lebo kubwa hapa Bongo kama WCB ya Diamond Platnumz, Kings Music ya Alikiba, Konde Gang ya Harmonize zina wasanii ambao wanafanya aina moja ya muziki wa Bongo Fleva.

Katika hizo lebo ambazo zimejipambanua kama lebo kubwa Afrika Mashariki, hakuna rapa wanaofanya Hip hop au wanamuziki wanaojikita katika muziki wa Rhumba au dansi.

Sampa Music Africa ni lebo yenye maskani yake jijini Dar es Salaam, chini ya CEO, Charles Benedicto Halawa ikiwa imejidhatiti kuupa nguvu muziki wa Hip hop Tanzania katika levo ya kimataifa pamoja na Rhumba / Dansi.

Mpaka sasa Sampa Music Africa imesaini wasanii wakali wawili ambao ni Mfalme Pharao mkali wa Rhumba na rapa machachari K Flow ambaye katikati ya wiki hii ametangazwa kama msanii wa kwanza kwenye lebo hiyo.

Akizungumza na BT jana, Halawa amesema miongoni mwa mipango yake ni kuwekeza zaidi katika muziki mzuri ambao lebo kubwa zimeshindwa kufanya.

"Sampa Music Africa ni kampuni yenye lengo la kukuza vipaji na kutoa ajira kwa vijana kupitia sanaa hii ya muziki ikiwa kama biashara, ni lebo yenye timu kubwa ya watu wengi wenye uwezo wa kuhakikisha kila kitu kinaenda kama kinavyo pangiliwa tupo na maprodyuza, Mameneja, waongozaji na vifaa vya muziki vyote," amesema

Ameongeza "Niwape moyo wasanii wote wanao pambania ndoto zao nakuamini juu ya vipaji vyao kwamba wasikate tamaa Sampa Music Africa ipo kwa ajili ya kila msanii mwenye kipaji cha kweli,"

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ONANA ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United inapania kumnunua mlinda mlango wa Cameroon na Inter Milan, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27, huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa Mhispania David de Gea mwenye miaka 32 kuondoka Old Trafford msimu huu wa joto. (***90 min***)

### COSTA NAE AWANIWA

MANCHESTER United pia inamfuatilia kipa wa Porto na Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa miaka 23 na kipa wa Brentford na Hispania, David Raya mwenye miaka 27, kama mbadala wa David de Gea. (***Sky Sports***)

### FEDERICO AWINDWA

KLABU ya Juventus imeweka dau la pauni milioni 52 kwa Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 25, huku Liverpool ikimtaka fowadi huyo wa Italia, ambaye pia anazivutia Bayern Munich na Paris Saint-Germain. (***La Gazzetta dello Sport***)

### PHILLIPS ANYATIWA

KIUNGO wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27, ambaye hapendelewi na Manchester City, ananyatiwa na Bayern Munich. (***Bild***)

### BREMER ATOLEWA MACHO

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtolea macho mlinzi wa Juventus na Brazil, Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 26, huku kocha mpya Ange Postecoglou akitaka kuimarisha safu yake ya ulinzi. (***Telegraph***)

### RICE NA ARSENAL

KLABU ya West Ham inaamini kwamba ofa ya tatu ya Arsenal ya karibu pauni milioni 100 kwa nahodha wao Declan Rice mwenye umri wa miaka 24 iko karibu huku mpango wa uhamisho wa kiungo huyo wa kati wa England ikikaribia kukamilika. (***Mail***)

### AZPILICUETA KWENDA INTER

MLINZI wa Hispania, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 33 anatarajiwa kuondoka Chelsea kwa uhamisho wa bure na tayari amekubali mkataba wa miaka miwili katika klabu ya Inter Milan baada ya kukataa ofa kutoka kwa Bayern Munich. (90 min)

### GALLAGHER AWANIWA

KLABU ya Borussia Dortmund inaweza kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, kama mbadala wa Jude Bellingham. (***Bild via Caught Offside)***

### SILVA ATAKIWA

KOCHA wa Fulham, Marco Silva mwenye umri wa miaka 45 hatakubali kubadilishwa na ofa ya fedha nyingi ya kuinoa Saudi Arabia huku Al Hilal wakimtaka kocha mkuu wa Ureno. (***Sun***)


### ZAHA AVUTIA LAZIO

MSHAMBULIAJI wa Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 30 anavutiwa na Lazio huku mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwezi huu. (***Sky Sports Italia)***

### LAVIA AWINDWA

ARSENAL imeripotiwa kufikia makubaliano ya maslahi binafsi na kiungo wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19 kutoka klabu ya Southampton. (***Football insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BUSQUETS AMFUATA MESSI MAREKANI

**NEW YORK,** Marekani

### ●●● MLS imetangaza kiungo huyo wa zamani wa Kimataifa wa Hispania atajiunga na...

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Sergio Busquets atajiunga na mchezaji mwenzake wa zamani Lionel Messi katika klabu ya Inter Miami FC msimu huu wa joto.

**Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS, imetangaza kuwasili kwa mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii.**

Mkataba wa Busquets na Barca unamalizika mwishoni mwa Juni na, baada ya kutangaza uamuzi wake wa kumaliza miaka 18 ya kukaa pale Spotify Camp Nou, amekuwa akitafakari kuhusu ofa kutoka Marekani na Saudi Arabia.

Vyanzo pia vimeiambia ESPN kwamba beki wa kushoto wa Barca, Jordi Alba pia amepokea nia kutoka kwa Miami na atafanya uamuzi juu ya mustakabali wake katika wiki zijazo baada ya kushinda kombe la Ligi ya Mataifa ya UEFA akiwa na Hispania.

Busquets mwenye umri wa miaka 34, alifanya mazungumzo na timu za Saudi Al Nassr na Al Hilal katika wiki za hivi karibuni lakini akachagua ofa ya Miami.

Ataunganishwa tena Florida Kusini na mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mara saba Messi, ambaye alitangaza nia yake ya kuhamia MLS mapema mwezi huu baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Paris Saint-Germain.


Busquets na Messi walitumia miaka 13 wakicheza pamoja kwenye kikosi cha kwanza cha Barca kabla ya kuhamia Paris mwaka 2021. Wawili hao wameendelea kuwa marafiki wa karibu tangu wakati huo.

Busquets aliichezea Barca mechi 722 kwa jumla, akishinda mataji tisa ya ligi na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia ameichezea Hispania mara 143, akishinda Kombe la Dunia mwaka 2010 na Ubingwa wa Ulaya mwaka 2012 kabla ya kutangaza kustaafu soka la kimataifa baada ya Kombe la Dunia mwaka jana nchini Qatar.

Busquets na Messi bado wanaweza kuunganishwa Miami na Alba, ambaye alifikia makubaliano na Barca mwezi uliopita kumaliza mkataba wake ambao ulikuwa inamalizika 2024.

# KLABU BINGWA YA DUNIA KUSHIRIKISHA TIMU 32




**NEW YORK,** Marekani

MAREKANI itakuwa mwenyeji wa Kombe la Klabu bingwa ya Dunia mwaka 2025, ikiwa ni mara ya kwanza kwa michuano hiyo ya Shirikisho la soka la kimataifa, FIFA, kuwa na timu 32.

Real Madrid, Manchester City na Chelsea tayari zimepata nafasi kama washindi wa hivi majuzi wa Ligi ya Mabingwa Uaya kwa safu iliyopanuliwa ya mashindano ambayo yanatarajiwa kujaribu viwanja na shughuli mwaka mmoja kabla ya Kombe la Dunia la 2026.

Marekani itakuwa mwenyeji wa Kombe kwa ushirikiano na Canada na Mexico, na FIFA bado inaweza kutoa baadhi ya michezo ya Kombe la Dunia la klabu hizo.

Kombe la Dunia la klabu litafanyika Juni hadi Julai 2025.

Marekani ilichaguliwa kuwa mwenyeji wakati wa mkutano wa mtandaoni wa Baraza la FIFA.

FIFA ilisifu "nafasi ya Marekani kama kiongozi aliyethibitishwa katika kuandaa matukio ya kimataifa na kwa sababu itaruhusu FIFA kuongeza ushirikiano na utoaji" wa mashindano ya 2026.

Seattle Sounders FC pia itashiriki Kombe la Dunia la Klabu kama bingwa wa 2022 wa eneo la kandanda la Amerika Kaskazini, Concacaf.

Timu maarufu za Ulaya zimetembelea Marekani kwa michezo ya kirafiki ya kujiandaa kwa msimu mpya, lakini mashindano ya klabu yaliyopanuliwa yatawapa mashabiki nafasi adimu kuona timu 12 kati yao zikicheza michezo ya ushindani.

FIFA ilisema Machi njia ya msingi ya kufuzu kwa klabu ilikuwa kushinda ubingwa wa bara katika kipindi chochote cha miaka minne kutoka 2021 hadi 2024 katika mashirikisho makuu matano: Afrika, Asia, Ulaya, Amerika Kaskazini na Amerika Kusini.

Ulaya yenye timu 12 na Amerika Kusini ikiwa na sita ndio mabara pekee yenye timu nyingi.

Nafasi za ziada zinatarajiwa kutolewa kulingana na viwango vya timu kulingana na matokeo ya muda wa miaka minne katika mashindano ya bara.

Kombe la Dunia la klabu la sasa la timu saba kwa mabingwa wa bara linalochezwa kila msimu huleta mvuto mkubwa na FIFA kwa muda mrefu imekuwa ikitaka kuandaa mashindano ya ukubwa kamili kila baada ya miaka minne.

Timu nyingine ambazo tayari zimefuzu kwa Kombe la Dunia la Klabu 2025 ni: Palmeiras (Brazil), Flamengo (Brazil), Monterrey (Mexico), Leon (Mexico), Al-Ahly (Misri), Wydad Casablanca (Morocco), Urawa Red Diamonds (Japan). ) na Al Hilal (Saudi Arabia).

## Man United yakomaa na Mount

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inatayarisha ofa ya tatu na inayoweza kuwa ya mwisho kwa kiungo wa Chelsea Mason Mount, vyanzo vimeiambia ESPN.

Ofa yao mpya bado haijakamilishwa lakini vyanzo vinadokeza kuwa inatarajiwa kuwa kati ya pauni milioni 55 na pauni milioni 60.

Kikosi cha Erik ten Hag kimekataliwa maombi mawili rasmi ya mchezaji huyo katika siku za hivi karibuni.

Awali Chelsea ilikuwa ikishikilia pauni milioni 70 na ingawa vyanzo vinapendekeza kwamba klabu hiyo inapunguza msimamo wao juu ya hesabu hiyo.

Mount anataka kuhamia Old Trafford na anatumaini makubaliano yanaweza kufikiwa. Amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake Chelsea, ambapo mazungumzo ya kuongezwa kwa mkataba huo yalikwama miezi kadhaa iliyopita.

Chelsea wako chini ya shinikizo la kukamilisha mikataba kabla ya Juni 30 ili kusaidia kufuata kanuni za haki sawa ya kifedha baada ya kutumia zaidi ya milioni 650 kwa wachezaji katika mwaka wa kwanza kamili wa umiliki wa Todd Boehly na Clearlake Capital.

Hata hivyo, hali hiyo imekuwa shwari, huku mambo kadhaa yakitarajiwa kukamilishwa ikiwa ni pamoja na uhamisho wa Kai Havertz kwenda Arsenal, Mateo Kovacic kujiunga na Manchester City, pamoja na Kalidou Koulibaly, Edouard Mendy na Hakim Ziyech kuhamia klabu za Saudi Arabia.



# Benitez akubali kuinoa Celta Vigo

**MADRID,** Hispania

RAFA Benitez amefikia makubaliano ya awali ya kuifundisha klabu ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Celta Vigo, klabu hiyo ya Hispania ilitangaza Ijumaa.

Benitez mwenye umri wa miaka 63 anachukua nafasi iliyo wazi ya ukocha baada ya Carlos Carvalhal kuondoka katika klabu hiyo mapema mwezi huu kwa makubaliano.

Mhispania huyo amekubali mkataba utakaomweka klabuni hapo hadi Juni 2026.

"Klabu ya Real Celta imefikia makubaliano kimsingi na Rafa Benítez ili kocha huyo mzaliwa wa Madrid aweze kuiongoza timu katika mwaka huu wa kipekee na kampeni mbili zaidi," taarifa ya klabu ilisema.

"Pande zote mbili zina imani kwamba usajili utafanyika Julai, pamoja na kuanza kwa maandalizi ya msimu wa timu."

Benitez alikuwa ameacha kazi tangu kutimuliwa na Everton Januari 2022 baada ya kuiongoza kwa miezi sita na nusu pekee.

Kocha huyo wa zamani wa Valencia anafahamika zaidi nchini England kwa kuiongoza Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2005.

Pia aliiongoza Chelsea kutwaa taji la Ligi ya Europa mwaka wa 2013 na Newcastle United kupandisha daraja hadi Ligi Kuu mwaka wa 2017.

Benitez, ambaye alishinda mataji mawili ya LaLiga na Kombe la UEFA akiwa na Valencia, pia amezifundisha Inter Milan, Napoli, na Dalian Professional ya Ligi Kuu ya China.

Mara ya mwisho kufundisha nchini Hispania ilikuwa ni Real Madrid msimu wa joyo mwaka 2015, ingawa miamba hao walimtimua miezi sita baadaye.

Benitez anarithi timu ya Celta ambayo iliokolewa kutoka kushuka daraja siku ya mwisho ya msimu kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya Barcelona kwenye uwanja wao wa Balaidos.

Klabu hiyo ilimaliza katika nafasi ya 13 kwenye msimamo, pointi tatu mbele ya Real Valladolid iliyoshuka daraja.



HABARI MICHEZO

# MASHABIKI NAMUNGO FC WASIFIA USAJILI WA NYONI

Na Adam Fungamwango

SIKU chachetubaadayauongoziwaNamungo FC kutangazakumchukuakiungomkongweErastoNyonikutokaSimba, mashabikiwatimuhiyowamepongezakwausajilihuo.

Mashabikihaowamesemaviongoziwaowamesikiakiliochaomashabikicha kuwatakawatafutewachezajiwenyeuwezonawazoefumkubwa.

WakizungumzakutokaRuangwamkoaniLindi, mashabikihaowamesemausajiliwaNyoni, umeonyeshakuwaviongoziwaowanadhamirayakuhakikishamsimuujaowanapatanafasiyakuchezamashindanoyakimataifa.

"Nipendekuwapongezaviongoziwetukwakumsajili Nyoni, wanatuonyeshakuwaklabuyetusasainawezakupambananakusajiliwachezajiwakubwa, nanimatumainiyetumsimuujaotutakuwavizurizaidiyamsimuhuu, huuniusajiliwakutupelekakumalizandaniyanafasinnezajuututachezemichuanoyakimataifakamamsimuuleambaotulifikahadihatuayamakundi," alisema Allan Alfonce.

Aidha, RamadhaniSeif, shabikiwatimuhiyokutokaRuangwa, alisemaNyoninimchezajimkubwa, hivyoanaaminiatakujakuletakitutofautinauzoefundaniyakikosi.

"TumefurahikusajiliwaNyoni, nimchezajimkubwanaametokaklabukubwa, tuaaminikuwaatakujakuongezauzoefukwenyekikosi, siyokazinyepesi, wanatuonyeshakuwasasawanawezakusajiliwachezajiwenginewakutufikishambali," alisema.

Hatahivyo, shabiki Amos Ezekiel amewaombaviongoziwaNamungokutoishiakumsajiliNyoninawanatakiwapiakusajiliwachezajikutokanjeyanchiwenyeuwezokupambaniatimu.

"Hakunamtuambayeanatakamatokeomabayakwenyeklabuyake, tumefurahiNyonikusajiliwa, lakinisisikamamashabikiwaNamungotunatakakuonainafanyausajiliwakimataifazaidi, ndiyowachezajiwandaniwananafasiyao, lakiniwachezajikutokanjenimuhimuzaidi," alisema Ezekiel.

NyonialitambulishwanaklabuhiyO, sikumojatubaadayakumalizamkataba wake naklabuyakeyaSimbaaliyoitumikiakwamiakasitakuanziamwaka2017 akitokeaAzam FC.



Mchezaji wa mpira wa kikapu, Felix Ephraim, akifunga goli wakati walipokuwa wakifanya mazoezi ya mchezo huo na wenzake katika Viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Chama, Kanoute kuongezewa mkataba Simba

INATOKA UK. 24

kikosi cha wachezaji ambao watakuwa na msaada kwa klabu huku akitaka kila namba iwe na wachezaji wawili wenye uwezo unaofanana au kupishana kidogo tofauti na ilivyo sasa kwenye kikosi chake.

Robertino aliacha ripoti yake kwa uongozi wa timu hiyo akitaja maeneo ambayo anataka yaboreshwe kwa kusajili wachezaji wengine.

Katika hatua nyingine, inaelezwa klabu hiyo ipo kwenye hatua za mwisho za kumsainisha golikipa raia wa Brazil Caique Luiz Santos kutoka kwenye klabu ya Ypiranga FC inayocheza Seria C nchini humo.

Kipa huyo atasajiliwa kuziba nafasi ya Beno Kakolanya aliyetimkia Singida Fountain Gate baada ya kumaliza mkataba wake Simba, pia anatajwa kuja kuwa chaguo la kwanza ndani ya kikosi cha Simba wakati huu ambao watamkosa golikipa wao namba moja Aishi Manula anayeuguza majeraha baada ya kufanyiwa upasuaji wa nyama za paja mwezi uliopita nchini Afrika Kusini.

Simba pia ilitajwa kuwa kwenye mazungumzo na magolikipa wengine Issa Fofana wa Al Hilal ya Sudan, na Alfred Muderekeza wa Vipers ya Uganda.

## *Yanga ilivyovuna faida...*

INATOKA UK. 24

Aidha, Hersi alisema uongozi wake umekuja na mfumo mpya wa kuongeza wanachama kwa kuingia makubaliano na Benki tatu za NMB, CRDB na NBC kwa ajili ya kuwapa urahisi wanachama walioko mikoani kujisajili kupitia benki hizo.

Alisema kupitia mfumo huo wa usajili wa wanachama na idadi kubwa ya wanachama watakaojitokeza, watakuwa na thamani ya dhamana ya kupata mkopo wa kujenga uwanja wao na klabu kumiliki miundo mbinu yake.

"Niwahakikishie mashabiki na wanachama wa Yanga, hatutamaliza muda wetu hadi tumalize ujenzi wa uwanja wetu wa Kaunda," alisema Rais huyo wa Yanga.

**Kauli ya Serikali**

Katika hatua nyingine Mgeni rasmi katika Mkutano huo, Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila aliyewasili eneo hilo 5:50 aliwataka Wanayanga kujenga uimara wa klabu hiyo ili kusonga mbele na kuwasapoti viongozi wenye maono ya kuleta maendeleo ya klabu hasa kwenye kumiliki miundo mbinu ikiwemo Viwanja na kuongeza vyanzo vya mapato.

"Niwaombe tuongezee ushirikiano ili kuwa na klabu bora, figisu katika mpira haziwezi kufika popote, viongozi wanapokosea wanatakiwa kuambiwa ukweli ili kujiweka sawa na kuweza kuendesha klabu vizuri," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa ni muhimu Yanga pamoja na klabu zingine kutumia vizuri amani ya nchi kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano ya kimataifa kwa kuitangaza na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

"Serikali tuko pamoja na Yanga na klabu zingine kuhakikisha zinafanikiwa kufanya vizuri, nimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kuonyesha mahaba yake katika michezo hasa katika soka kwa zile hamasa alizozitoa kwa hizi klabu katika michuano ya kimataifa na timu ya Taifa," alisema Chalamila.

Kuhusu ushabiki, Chalamila alisema kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa kimichezo alikuwa shabiki mkubwa wa Yanga na kwa kuwa amepewa cheo hicho analazimika kusimama kama baba kwa kutokuwa upande wowote miongoni mwa klabu za Dar es Salaam

"Lakini inapotokea nimeteleza kimahaba naomba wanisamehe, ila mke wangu nyumbani ni Simba na tutakuwa pamoja katika jambo hilo kwa sababu ya cheo changu kunilazimu kuwa sehemu zote," alisema Chalamila.

**Huyu hapa kocha wa Yanga**

Kocha aliyetangazwa na Hersi jana Miguel Angel Gamondi (59) ni moja ya makocha wenye uzoefu mkubwa na soka la Afrika.

Kocha huyo licha ya kutokuwa na taji lolote kubwa Afrika, ni kocha mwenye uzoefu aliyefundisha timu nane zenye majina Afrika. Miongoni mwa timu hizo ni Wydad Casablanca ya Morocco, Esperance ya Tunisia, Mamelodi Sundowns na Platinums FC za Afrika Kusini, CR Belouizdad na USM Alger za Algeria na Al Ahly Tripoli ya Libya.

Historia ya kocha huyo inaonyesha kuwa ameifundisha timu moja tu ya nchini kwao Argentina ambayo ni Racing Club de Avellaneda mwaka 1998 hadi 1999 na ilikuwa ni mara ya kwanza kwenye karia yake ya ukocha.

Historia ya kocha huyo inaonyesha kuwa ameifundisha timu moja tu ya nchini kwao Argentina ambayo ni Racing Club de Avellaneda mwaka 1998 hadi 1999 na ilikuwa ni mara ya kwanza kwenye karia yake ya ukocha.

Amewahi pia kuwa kocha msaidizi wa timu ya taifa ya Burkina Faso mwaka 2001 mpaka 2002.

## Tanzania yaangukia pua Kikapu Afrika

Na ShufaaLyimo

LICHA yakuwaMwenyejiwamashindanoyampirawakikapuyakufuzufainalizaAfrikakwawachezajiwandanikandawatano (FIBA Afro CAN), Tanzania imeshindwakufanyavizurinakujikutaikishikanafasiyanne.

KatikamashindanohayoyaliyomalizikajuzikwenyeUwanjawandaniwaTaifa, timuyaTaifaRwanda imeibukabingwawamashindano hayokwa wanaume na kufuzu kwa fainali hizo.

Rwanda imeibukabingwabaadayakuichapaBurundi pointi 70-48 katikamchezowakutafutanafasiya kwanza kuwakilishakandahiikatikamichuanoyaAfroCan.

Kwamatokeohayo Burundi imeshikanafasiyapili ,hukuSudaniyakusuniikiwanafasiyatatu ,wakatiElitreaikimalizianafasiyatano.

AkizungumzanaNipashe marabaadayakumalizikakwamashindanohayo, AfisamichezowaBaraza la Michezo la Taifa (BMT) Allen Alex,alisema kuwaSerikaliitaendelea kuwekanguvuilikuhakikishamchezohuounapigahatua.

Alisemakwamwakahuuwalisaidiamashindanohayona watakaapamojakuonawanahitaji ninikwalengo la kuboreshailiwavukehatuawaliyofikiamwakahuukwenyemashindanohayo.

"Tumeonaleo(juzi )Vijanawamepambananawatanzaniawamejitokezakwawingi kuungamkonotimuyetu, alisema Alex.

Aidha, RaiswaShirikisho la MpirawaKikapuTanzania(TBF) RwehaburaBarongo,alisemakuwawatakwendakufanyatathminiyaupungufuuliojitokeza katikamashindanohayo .

" Kwasasatunakwend akufanyatathmini,tuna mashindanomengineyakimataifamweziNovemba tutaandaa program nakufanyamaandalizimakubwailikufanyavizurisikuzijazo," alisemaBarongo

KwaupandewaKochawa Tanzania, RobartManyerere,alisem akunaajayakuwekezakwenyemiundombinu ilikusaidiakukuzamchezohuo.

Piaalisemalazimakuandaawachezajiwenyevipajimashuleniwatakaopatikanakupitiamichezoya Umisetana Umitashumta.

Michezo
Jumapili Juni 25, 2023
Nipashe



## Busquets amfuata Messi Marekani



Rais wa Klabu ya Yanga, Hersi Saidi (kwenye kipazasauti) akizungumza katika Mkutano Mkuu wa klabu hiyo uliofanyika jana Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Yanga ilivyovuna faida ya nusu bilioni msimu 1

## ●●● Yamtangaza mrithi wa Nabi, amezinoa timu kubwa za Afrika...

**Na Saada Akida**

KLABU ya Yanga imetangaza kutengeneza faida ya zaidi ya shilingi milioni 500 msimu uliopita kutokana na kufanya vizuri kwenye mashindano ya ndani na ya kimataifa.

Pia jana kupitia mkutano mkuu wa klabu hiyo ilimtangaza mrithi wa kocha Nasreddine Nabi ambaye ni Muargentina, Miguel Angel Gamond aliyepewa rasmi mikoba ya kuifundisha timu hiyo.

Akizungumza mbele ya wanachama wa klabu hiyo kwenye Ukumbi wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said, alisema msimu uliomalizika waliingiza kiasi cha Sh. bilioni 17.8 kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo viingilio, wadhamini na faida ya ushiriki mashindano ya kimataifa ambako walifika mpaka hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hersi alisema kwa msimu huo pia walitumia Sh. bilioni 17.3 katika matumizi mbalimbali ya timu hiyo na kufanya kubaki na faida ya shilingi milioni 500.

Huku akishangiliwa na wanachama kwenye mkutano huo wa masaa matatu ulioanza saa 5:23 asubuhi na kumalizika saa 8:22, Hersi alisema kwa msimu ujao 2023/2024, klabu hiyo imeweka bajeti ya Sh. bilioni 20 huku tayari wakiwa na uhakika wa kukusanya Sh. bilioni 14.3.

Alisema watakuwa na pungufu ya Sh. bilioni sita ili kufikia bajeti hiyo na wana uhakika kwa ushirikiano wa viongozi, wanachama na wadhamini wao watafanikiwa kupata fedha zote.

"Upungufu huu kwa bajeti yetu ya msimu ujao ni jukumu letu wote Wanayanga kuzipata na kuhakikisha tunapandisha thamani ya klabu yetu ili kuvutia baadhi ya taasisi na matajiri kujitokeza kudhamini timu yetu," alisema Hersi na kuongeza,

Tunahitaji kufanya usajili mzuri kulingana na mahitaji yetu kuendeleza pale tulipoishia kwa msimu huu baada ya kupata mafanikio ikiwemo kutetea mataji yetu yote matatu pamoja na kuiheshimisha nchini kwa kuleta medali ya fainali ya mashindano ya kimataifa," alisema Hersi

Alisema kama uongozi wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kuwaumiza wapinzani wao kwa kufanya vizuri zaidi kwenye ligi na mashindano ya kimataifa.

"Mafanikio tuliyoyapata msimu huu yamewaumiza sana wapinzani wetu, tunawahakikishia wanachama wa Yanga msimu ujao tutaendelea kufanya vizuri na ikiwezekana vizuri zaidi ya msimu huu ili tuendelee kuwaumiza," alisema Hersi na kushangiliwa na wanachama wa klabu hiyo waliofurika kwenye mkutano huo wa mwaka.

INAENDELEA UK. 23

## Chama, Kanoute kuongezewa mkataba Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kukiwa na taarifa ya winga Pape Sakho kutaka kutimkia Ubelgiji anapotakiwa na klabu ya KVC Westerlo, Uongozi wa Simba upo mbioni kuwaongezea mikataba wachezaji wake Clatous Chama na Sadio Kanoute.

Taarifa zilizopatikana kutoka magazeti na mitandao mbalimbali nchini Ghana na Senegal zinasema kuwa klabu hiyo ya Westerlo inamtaka Sakho anayeichezea pia timu ya taifa ya Senegal kwa dola za Kimarekani 500,000 (Zaidi ya Sh.1 bilioni)

Hata hivyo inaelezwa Sakho ameugawa uongozi wa Simba ambapo wapo wanaotaka auzwe na kuchangamkia fedha hizo lakini wengine wanataka aendelee kuwemo kikosini kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano ya ndani na ile ya kimataifa.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo Murtaza Mangungu, juzi alisema kati ya wachezaji ambao wataachana nao ni wale ambao wamemaliza mikataba na hawapo kwenye mipango ya timu, lakini wapo wengine wanaotakiwa na timu nyingine na wenyewe wanataka kwenda kusaka malisho sehemu nyingine na wengine wataachwa ili kupisha wachezaji wengine.

Alisema wapo mbioni kuwapa mikataba mipya wachezaji wao nyota wanaomaliza mikataba yao na wale waliobakiza muda mchache kumaliza mikataba.

"Mazungumzo yanaendelea kwa wachezaji wote tunaowahitaji na ambao mikataba yao inaenda ukingoni wakiwemo hao akina Chama, Kanoute, lengoni kuwa na kikosi kizuri kitakachorejesha mataji yetu yote," alisema.

Kuhusu Sakho alisema anasikia tu kwenye mitandao kutakiwa Ubelgiji lakini kama ofa itawafikia mezani watakaa kujadiliana na kutoa maamuzi juu ya mustakabali wa nyota huyo kutoka Senegal.

Kabla ya kuondoka mapumzikoni, Kocha wa Simba Roberto Oliveira 'Robertinho' alisema anataka kutengeneza

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >